# Nipashe

Alhamisi Novemba 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580411

The Guardian digital · nipa...media.com · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


**MAKAMU** Rais GGM avipongeza vyombo vya habari vya IPP

UKURASA 3



**DK. TULIA** awaonya wanaume kwa kuwapiga wake zao

UKURASA 4




UKURASA 11

**UBUNGE VITI MAALUM:**

# Mdee, wenzake sasa kikaangoni

**WAITWA** kujieleza Kamati Kuu CHADEMA kesho, Prof. Safari ataja adhabu yao iwapo...*Endelea Ukurasa wa 2*




Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kutowatambua wabunge wa viti maalum wa chama hicho, walioapishwa Bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**KIBANO WATAKAOUZA SARUJI ZAIDI 20,000/-**

MKUU wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, amepiga marufuku wafanyabiashara wa saruji kuuza bidhaa hiyo kwa zaidi ya Sh. 20,000 na watakaokiuka...

UKURASA WA 5

**AOMBA MSAADA WA FEDHA KUWEKEWA MASHINE YA MOYO**

JOYCE Nasolwa, mkazi wa jijini Arusha mwenye tatizo la moyo, anaomba msaada wa Sh. milioni 14.9 kwa wasamaria wema, ili kuwekewa...

**Maofisa TRA matatani tuhuma za rushwa**

UKURASA 3

# Laiser mwingine aibuka bilionea

UKURASA 2

**MICHEZO** MOROCCO ATOA HESABU ZA KUWAMALIZA WASUDAN CAF UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Laiser mwingine aibuka bilionea wa madini

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

MCHIMBAJI mwingine mdogo wa madini kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai, Gabriel Sendeu Laiser, ameibuka bilionea baada ya kupata madini ya ruby yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.7.

Laiser amepata madini hayo kupitia mgodi wake ulioko eneo la Mundarara, Longido mkoani Arusha. Akizungumza jana na wataalamu na watendaji wa sekta ya madini waliotembelea mgodi huo, Laiser alisema mafanikio hayo ni matokeo ya hatua zinazochukuliwa na serikali kuwajengea wachimbaji wadogo mazingira mazuri ya uchimbaji.

Laiser ni kijana wa pili kutoka jamii ya wafugaji wa Kimasai kuibuka bilionea kupitia madini katika kipindi kifupi. Wa kwanza akiwa ni kijana mwingine Saniniu Laiser (hawana undugu) ambaye alipata kilo zaidi ya 11 za madini ya Tanzanite yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne.

Kutokana na mafanikio hayo, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuwathamini wachimbaji wadogo na kuwatetea, hatua ambayo alisema imechangia mafanikio yake.

Hata hivyo, amewashauri wachimbaji wenzake wadogo kuendelea kuchimba bila kukata tamaa kwa kuwa kazi hiyo inahitaji uvumilivu na kujitoa kwa dhati na si rahisi kama wengi wanavyofikiria.

"Hapa nimepambana sana, nimewekeza sana na nimekopa mikopo mingi. Ninachoshukuru ni kwamba hata walionikopesha wamenivumilia sana japo na mimi nilionyesha uadilifu wa kurejesha kwa hiyo kwa kweli kazi hii ni nzuri, lakini pia ni ngumu na inahitaji uvumilivu mkubwa," alisema.

Mmoja wa wachimbaji wadogo katika eneo hilo, Lekule lazier, ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Longido, alisema kuna uwezekano wa kunufaika na rasilimali hiyo kama taasisi za fedha zitaona umhimu wa kuwasaidia kwa kuwapa mikopo ya masharti nafuu na ya muda mrefu."Wachimbaji wote wanatamani kuwa mabilionea. Wanataka kuchimba, lakini uwezo wa mitaji ndilo tatizo. Kama benki zitaamua kuwekeza kwa wachimbaji wadogo, kwa kweli tutapata mabilionea wengi sana," alisema.

Nao Alfred Antony, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo na Jeremia Simeon, Mwenyekiti wa Wachimbaji wa Kati, walisema wachimbaji wote wadogo wako tayari na wana ari ya kuchimba na wanafurahi kuona serikali inaendelea kuwaboreshea mazingira, lakini tatizo kubwa walilo nalo ni mitaji na vitendea kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliwataka wachimbaji wadogo kuona umuhimu wa kuunganisha nguvu ili kupata vitendea kazi vya kuwawezesha kuchimba kisasa zaidi na kunufaika na madini ambayo sasa yamewekewa utaratibu mzuri wa kuhakikisha yanawanufaisha wazawa.

Mwaisumbe pia aliwashauri wachimbaji wadogo kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali ikiwamo kudhibiti utoroshaji wa madini ili yaendelee kuwanufaisha wananchi na taifa kwa ujumla.

Ofisa Mkazi wa Madini Mkoa (RMO) wa Arusha, Aidan Muhando, alimpongeza Laiser kwa kuona umuhimu wa kufanya uchimbaji kwa uwazi na kufuata sheria na taratibu zilizowekwa hatua ambayo imemwezesha kupata mafanikio yeye mwenyewe, serikali na jamii kwa ujumla.

Aliwataka wachimbaji wengine wenye leseni za kuchimba katika maeneo hayo ambao hawajaanza, kuhakikisha wanaanza kuchimba ili kuongeza uzalishaji.



Mchimbaji mdogo wa madini ya ruby, wilayani Longido, mkoani Arusha, Gabriel Sendeu Laiser, akionyesha sehemu ya tani 5.4 za madini hayo zenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 alizopata katika mgodi wake, eneo la Mundarara, wilayani humo jana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Mdee, wenzake sasa kuwekwa kikaangoni

**Na Mwandishi wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kuwa kesho kitawaweka kiti moto wabunge 19 wa Viti Maalum waliokubali kuapishwa kwa madai ya kutofuata taratibu za chama hicho.

CHADEMA pia imekana kuhusika katika mchakato wa kupata majina hayo, huku ikitilia shaka kuachiwa Novemba 22, mwaka huu, kwa haraka kwa kiongozi wa Baraza la Vijana (BAVICHA) aliyesota rumand siku 133 na kuapishwa Novemba 23. Kinahoji ni lini alijaza fomu, zikatiwa saini na kupigwa muhuri wa mahakama. Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa fomu za orodha ya wabunge hao zilizopelekwa CHADEMA zilikuwa hazijajazwa na kuna sehemu lazima zitiwe saini naye na kwamba hajawahi kutia saini fomu yoyote.

**KAMATI KUU YA DHARURA**

Kutokana na sakata hilo, alisema CHADEMA imeitisha Kamati Kuu Maalum na kwamba watawaandikia wahusika ili kisitokee kisingizio chochote cha kuitwa.

"Natawatangaza kupitia vyombo vya habari kwa wanachama wetu 19 kufika makao makuu ya chama bila kukosa siku ya Ijumaa saa 2:00 asubuhi, Makao Mkuu ya chama kutoka popote walipo.

"CHADEMA inaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Maadili na Itifaki ya chama, ambayo imetoa mfumo kuwa hatua zisichukuliwe bila wahusika kuitwa, kujieleza, na kwa kuwa ni jambo la dharura, tutatumia utaratibu wa dharura kulishughulikia." alisema.

"Mimi kama Katibu Mkuu hakuna fomu yoyote ya mtu yoyote niliyowahi kuijaza popote kuthibitisha uteuzi wa yeyote, hii fomu ina sehemu B ya tamko la kisheria la mgombea wa Viti Maalum, linajazwa linakwenda na kiapo cha Hakimu, mchakato huo haukufuatwa.

"Kilichofanyika ni biashara haramu ya kughushi ambayo imehusisha mifumo mbalimbali, ikiwamo waliokwenda kuapa bila ridhaa ya chama, bila baraka za chama na bila kupitishwa na kwa mamlaka halali za chama, CHADEMA haijafanya uteuzi wowote na mchakato huu hautapitiwa kwa namna yoyote ile," alisisitiza.

**MBOWE HAHUSIKI**

Alisema kauli iliyotolewa kuwa waliokwenda kuapa wana baraka za Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, si za kweli na kwamba waliokwenda waliamua wenyewe.

"Hakuna baraka zozote za Mwenyekiti Mbowe, tutatoa kauli ya kiongozi wa CHADEMA, tutajua aliyebariki orodha hiyo bila vikao vya kikatiba vya chama, bila mamlaka halali. Hiki ni chama cha Demokrasia, ni vyema tuelezwe ni kikao gani kilikaa na kufanya maamuzi (uamuzi). Waliokwenda walijiteua na kushirikiana na mifumo kwenda kuapa kuhalalisha ubatili, usaliti na uharamu," alisema.

**MAWASILIANO CHADEMA NA NEC**

Mnyika alibainisha kuwa mawasiliano yake na NEC ilikuwa barua ya Novemba 9, mwaka huu, kwenda kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, ambayo iliandikwa baada ya kunukuliwa kusema CHADEMA imeshawasilisha orodha na imepeleka majina na kuwasilisha bungeni.

Baada ya barua hiyo, NEC iliwajibu CHADEMA kuwa: "Barua ya Novemba 14, 2020 ilikuwa na kichwa cha habari uteuzi wa wabunge wa Viti Maalum, pamoja na mambo mengine, katika barua iliyotiwa saini na Mkurugenzi wa NEC walikiri kutopokea orodha kutoka CHADEMA na kutaka kuwasilisha orodha na fomu namba nane D."

**ALIYESOTA RUMANDE**

Mnyika alisema kuna ishara zilionekana ikiwamo kiongozi wa BAVICHA, Nusrat Hanje, aliyesota mahabusu kwa siku 133 na jana Mahakama Kuu ndiyo ilikuwa inakutana kukata rufani. Alisema Novemba 23, mwaka huu, alitolewa gerezani na alionekana miongoni mwa waliokula kiapo cha kuwa mbunge, jambo linalozua maswali mengi.

**AHOJI UHARAKA**

"Spika Job Ndugai anasema alipelekewa majina Novemba 20, mwaka huu, Katiba na sheria zinasema kabla ya NEC kuteua inakuwa na orodha na fomu. Hanje aliyetolewa gerezani Novemba 23, fomu yake alijaza lini? Hakimu aliyemwapisha alikuwa wapi? Mambo yanayodhihirisha wazi kulikuwa na nguvu ya ziada, lengo kutaka kufifisha ajenda ya uchaguzi mkuu ambao ulikuwa na kasoro mbalimbali," alisema.

**AWATULIZA WANACHAMA**

Mnyika alisema ni vyema Watanzania wakabaki kwenye mjadala wa uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu, na kwamba bado hawajabadili msimamo wao kuhusu uchaguzi huo ambao kasoro zake zilionekana.

"Nawahakikishia Watanzania kuwa chama hiki kitaendelea na kitakuwa salama, kitapita katika mchakato huu kikiwa na nguvu zaidi ya kujipanga kushika dola, historia ya CHADEMA masuala ya kuita viongozi wakubwa kwaita na kuchukua hatua za kinidhamu yalishatokea, na chama kilivuka salama na kuendelea kuwa matumaini ya Watanzania,"alisema.

Aidha, Mnyika alipotakiwa kueleza hatua zitakazochukuliwa, alisema uamuzi utatolewa na Kamati Kuu Novemba 27, mwaka huu.

**UHUSIKA WA KATIBU MKUU**

Alisema hadi sasa hana ushahidi wa kuhusika kwa ofisi ya Katibu Mkuu wa CHADEMA na kwamba anachofahamu ni wahusika waliokwenda kuapa, na kwamba mwenye ushahidi auwasilishe kwake.

Mnyika alisema viongozi wa chama hicho na chama cha ACT Wazalendo, alizungumza na waandishi wa habari mara baada ya uchaguzi na kueleza kuwa hawatatuma wawakilishi wao bungeni ikiwamo wabunge wa viti maalum, kutokana na kutoridhishwa na uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, Rais John Magufuli aliibuka kwa ushindi wa kura milioni 12.5 huku mpinzani wake wa karibu, Tundu Lissu, akipata kura milioni 1.9.

Novemba 10, mwaka huu, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, alisema wanachama watakaokubali viti maalum bila utaratibu wa chama watakuwa wamekubali kilicho haramu.

## GGM yavipongeza vyombo vya habari IPP

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais wa kampuni ya uchimbaji madini ya Geita Gold Mine (GGM), Simon Shayo, amevipongeza vyombo vya habari vya IPP kwa kazi kubwa ya kuhabarisha umma mambo mbalimbali kwa wakati yanayotokea ndani na nje ya nchi.

Katika ziara yake ya kikazi aliyoifanya jana katika vyombo vya habari vinavyomilikiwa na IPP, Shayo alipata fursa ya kuona teknolojia ya hali ya juu inayotumika kupeleka taarifa kwa jamii kupitia vipindi tofauti vinavyorushwa na kampuni hiyo.

Kwa upande wa kampuni ya IPP walipokewa na kuongozwa na Mkurugenzi Joyce Luhanga ambaye aliwatembeza maeneo mbalimbali ya kampuni hiyo.

Shayo akiwa ameambatana na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Stephen Mhando, alitembelea kampuni ya magazeti ya The Guardian Limited inayochapisha magazeti ya The Guardian, Nipashe na Nipashe Jumapili na kujionea uandaaji wa habari hadi uchapishaji unavyofanyika.

Pia alitembelea studio za ITV/Radio One, East Africa Radio/Television na Capital Radio ambako kote aliona utayarishaji wa vipindi, matangazo ya moja kwa moja na habari mbalimbali zinavyoandaliwa na baadaye kurushwa. Akizungumza baada ya ziara hiyo, Shayo alisema tangu vyombo hivyo vilipoanzishwa GGM imekuwa mdau mkubwa. "Kampuni yetu ilianza kufanya kazi Tanzania tangu mwaka 1999 na uzalishaji ulianza rasmi mwaka 2000. Tulikuta vyombo vya IPP tayari vimeanza kazi. Tumejifunza mambo makubwa katika ziara hii, tumeona teknolojia ya hali ya juu inayotumika katika uandaaji na urushaji wa habari," alisema.

Shayo alisema mafanikio ya miaka 20 ya kampuni yao ya uchimbaji wa madini yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na vyombo vya habari vilivyo chini ya IPP.

"Tumeshirikiana kwenye miradi mikubwa mfano kampeni ya "Kilimanjaro Challenges against HIV and AIDS' ambayo kila mwaka huwa tunapeleka watu kupanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kukusanya fedha za mapambano dhidi ya Ukimwi nchini. Wako waandishi wa vyombo hivi walioshiriki," alisema. Katika eneo hilo la Ukimwi, Shayo aliwataka vijana watafute taarifa sahihi na kuzitumia kwa usahihi na wakati wowote wanapoingia katika uhusiano wahakikishe unakuwa salama kwao.

Alisema wanafurahi wamekuwa na miaka 20 ya mafanikio kiuzalishaji, uwekezaji kwenye jamii na ajira ambapo wameajiri zaidi ya watu 5,000 na yote yanachagizwa na wadau vikiwamo vyombo vya habari na serikali kwa ujumla. "Nyie ni chaguo letu na tunafanya kazi kwa karibu kwa kuelimisha jamii, kutekeleza fursa zaidi za kuwezesha jamii inayotuzunguka ipate manufaa. Watu wengi wanaangalia ajira zinazotolewa na mgodi, lakini zipo fursa za kufanya biashara na mgodi kama kutengeneza bidhaa na kutuuzia," alisema.

Kuhusu kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambayo ilianza jana, Shayo alisema kampuni yao huhakikisha mtu yoyote anayefanya kazi kwao, utu wake unaheshimiwa bila ya kujali ni nani.

"Unyanyasaji wowote wa kijinsia kwetu ni uporaji wa haki za binadamu. Hata ukiwa ni wa lugha kwetu hauvumiliki. Pindi tunapouthibitisha tutaachana na mhusika akatafute sehemu nyingine ya kazi," alisema.



Dereva wa gari dogo akipita kwenye eneo la mabasi ya mwendo kasi katika Barabara ya Morogoro, Manzese, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC Tanga awasimamisha watumishi 8 TRA

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, amewasimamisha kazi watumishi wanane wa Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kwenye kituo cha mpaka wa Horohoro, wilayani Mkinga.

Uamuzi huo umekuja baada ya kuundwa kwa kamati ya uchunguzi kituoni hapo kwa madai ya watumishi hao kufanya kazi zao wakiwa na tuhuma mbalimbali ndani na nje ya kituo.

Kabla ya kutoa uamuzi huo Shigela aliishukuru kamati hiyo na kueleza kuwa tuhuma zilizokuwa zikiwakabili watumishi hao ni pamoja na malalamiko ya wafanyabiashara kuzuiwa mizigo na watumishi kuomba rushwa na kupitishwa kwa mifugo kwa njia za panya.

"Kwanza niishukuru sana kamati, kituo hiki cha Horohoro ndio kituo mama kwa upande wetu, lakini kuna baadhi ya watumishi wamekigeuza shamba la bibi, kila mmoja anafanya anavyotaka," alisema.

"Nataka kuwaambia wananchi serikali ya awamu ya tano haitaki kuona mwananchi anaonewa na mtumishi wala mtumishi anaonewa na mwananchi, tume imefanya kazi yake vizuri na imetoa majibu mazuri," aliongeza.

Aliwataja watumishi hao na vyeo kwenye mabano kuwa ni Edward Ndupa (Meneja wa forodha) mkoa wa Tanga, Bakari Athumani (Ofisa forodha Mfawidhi) wa kituo, Danda Hamis (Ofisa forodha msaidizi) na Azizi Dutiro (Ofisa forodha msaidizi) wa kituo.

Wengine ni Julius Asila (Ofisa forodha), Bakari Ngoso (Ofisa forodha msaidizi), Nicodem Kilahuzi (Ofisa mifugo) wa kituo na Michael Katamba (Ofisa mkaguzi wa TBS) wa kituo.

Akitoa taarifa ya kamati, Katibu wa kamati ya uchunguzi, Horombo Alexander, alisema kuwa uchunguzi umefanyika ndani ya kipindi cha miezi mitatu kuanzia Septemba 18 na kumalizika Novemba, mwaka huu.

Alexander alisema uchunguzi umebaini upungufu ambao mwingine ulianza tangu kuanzishwa kwa kituo hicho hasa kuhusu kupitisha mifugo kwa njia za panya kuingia nchi jirani ya Kenya.

"Ukiwauliza mifugo inapitishwa wapi hapa forodhani wanakwambia hawajui na kituo hiki hakijawahi kuingiza mapato ya mifugo licha ya kuwa inapitishwa kila siku kutoka Tanzania kwenda kuuzwa nchi jirani ya Kenya, huku mpakani hakuna wanachojua."

Alisema katika kituo hicho kimefungwa mashine za scanner ambayo baada ya kufanyia uchunguzi waligundua mashine hiyo hainasi madawa ya kulevya wala fedha bandia huku zikisimamiwa na watumishi wa TRA pekee.

"Baada ya kugundua upungufu katika scanner hii tumeona tuongeze watumishi wa idara nyingine kuja kusimamia nao, tumeleta hapa Idara ya Polisi, Usalama, Jeshi la Zimamoto, Uhamiaji, Afya na TRA yenyewe," alifafanua.

"Tumegundua madudu mengi katika kituo kwa upande wa mifugo ofisa wa kituo cha mifugo hana taarifa ya kueleweka isipokuwa ana kitabu chake chenye taarifa zake hashirikishi mtu," aliongeza.

Hata hivyo, katibu huyo aliiomba serikali kuwachukulia hatua kali watumishi wote waliohusika katika ubadhirifu wa mali ya taifa kwa maslahi yao binafsi.

NMB
Karibu yako

TAARIFA KWA UMMA

Mpendwa Mteja,

Tunapenda kukutaarifu, kuanzia tarehe 25 Disemba 2020 tozo zifuatazo zitatumika kwa huduma zilizo tajwa hapo chini.

| HUDUMA | | MABADILIKO |
|---|---|---|
| Kukataliwa Muamala wa Kutoa katika ATM (Salio Pungufu) | | SH 1,200 |
| Ada za kutoa Pesa ATM | Viwango | Ada (SH) |
| | 1,000 - 20,000 | 1,100 |
| | 20,001 - 50,000 | 1,200 |
| | 50,001 - 100,000 | 1,300 |
| | 100,001 – 200,000 | 1,400 |
| | 200,001 – 400,000 | 1,500 |

Kwa maelezo zaidi tafadhaili wasiliana nasi kupitia numba **0800 002 002** au kwa barua pepe: Hudumakwawateja@nmbtz.com

**Imetolewa na Utawala wa NMB Bank Plc.**

www.nmbbank.co.tz

# Tulia aonya wanaume kupiga wake zao

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, amezindua kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, huku akiwataka wanaume kuacha kuwapiga wanawake na kuwafanyia ukatili wa aina mbalimbali.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, jana, jijini Dar es Salaam, Dk. Tulia alisema jamii haipaswi kuwaona wanawake na watoto wa kike kama viumbe dhaifu, hivyo kuwanyanyasa kwa vipigo na kingono.

Dk. Tulia alisema wanawake ambao wamepewa nafasi kwenye nafasi za uamuzi, wameonyesha uwezo mkubwa kama ilivyo kwa wanaume, kutokana na ukweli huo, alisema hakuna sababu kwa jamii kuendelea na mtazamo hasi dhidi yao.

"Kwa nini umpige mwanamke? Kama wewe unasikia maumivu ukipigwa basi na mwanamke anasikia maumivu, hivyo hakuna sababu ya kumpiga mwanamke pengine kwa kuona kwamba ni mtu dhaifu asiyewezaa kujitetea," alisema Dk. Tulia.

Aliitaka jamii kutumia siku hizo 16 kutafakari na kuanzisha mijadala ni kwa namna gani nchi inaweza kuondokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuzungumza na wanafunzi vyuoni na mitaani ili waeleze yanayowakuta.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, alisema jibu sahihi la nini kifanyike kukomesha ukatili kwa jamii linatoka kwenye jamii yenyewe.

"Viongozi wa dini, taasisi zisizo za kiserikali wanawajibika kupambana na ukatili wa kijinsia na tuwalee watoto wetu katika maadili ambayo watatambua kuwa ukatili ni mbaya," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anna Kulaya, alisema shirika hilo na wadau wengine wataendelea kutoa wito kwa serikali kuanzisha mchakato wa kutunga sheria kwa ajili ya kupambana na ukatili wa kijinsia na mahakama za kifamilia.

Alisema wataendelea kutoa wito wa kuharakisha kupitiwa kwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1977, ili kuharakishwa usikilizwaji wa mashauri ya ukatili wa majumbani na kuongezewa ulinzi kwa wanawake.

"Ni ombi letu kwa Serikali Kuu na halmashauri zote kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kutokomeza ukatili na tunaishukuru Wizara ya Afya kwa kuendelea kusimamia utungwaji wa sera na miongozo thabiti," alisema.

# Wanafunzi UDSM wang'ara mashindano ya TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Kitanzania kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamekuwa miongoni mwa vinara wa fainali za Shindano la Dunia la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano la Huawei lililofanyika mwishoni mwa wiki.

Timu ya wanafunzi hao kutoka Chuo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (COICT) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, walifanikiwa kufika hatua hiyo ya mashindano kufuatia kuibuka vinara katika mashindano hayo miongoni ya mwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Shindano hilo linalenga kutoa jukwaa kwa vijana wenye vipaji kwenye TEHAMA kuonyesha uwezo wao, kushindana na kuwasiliana, kuhimiza utafiti wa TEHAMA, na kusaidia ukuaji wa mfumo thabiti wa TEHAMA.

Timu ya wanafunzi hao kutoka Watanzania iliundwa na wanafunzi Mpoki Abel Mwaisela, Hongo Kelvin, Henry Kihanga, Aghatus Biro, John Lazaro na Elisante Akaro.

Akizungumzia ushindi huo kwa niaba ya wenzake, Hongo kutoka Tanzania alisema: "Mashindano hayo ya Huawei pamoja na kuwajenga kiuwezo yamekuwa na tija kwao ikiwamo kuwapatia vyeti vya utambuzi kuhusu mafanikio yao katika taaluma hiyo."

Mafanikio ya wanafunzi hao yanatajwa kuwa ni kwa sababu ya kutambuliwa kwa jitihada za nchi za Afrika katika kujenga vipaji vipya kwenye sekta ya TEHAMA ambao watakuwa kichocheo katika kurejesha ustawi wa bara hili baada ya janga la COVID-19.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Huawei imesaini makubaliano ya ushirikiano na vyuo vikuu zaidi ya 10 vya Tanzania juu ya kuanzisha taaluma za TEHAMA za Huawei.

Profesa William Anangisye, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliwasifu wanafunzi hao kwa ushindi wao mkubwa na kuinua uwakilishi wa chuo hicho.

"Nawapongeza wanafunzi kwa ushindi. Huu ni ushahidi dhahiri wa ubora wa masomo kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho huwaandaa wanafunzi wake kuwa wabunifu katika sayansi na teknolojia. Chuo Kikuu kinathamini ushirikiano na Huawei katika kuziba pengo la maarifa ya TEHAMA kwa wanafunzi wetu, na nachukua fursa hii kuwahimiza sana wanafunzi wote kushiriki katika programu za Huawei," alisema Prof. Anangisye.

Hou Tao, Makamu wa Rais wa Huawei Ulimwenguni, aliangazia shauku ya kuvutia ya wanafunzi, ambayo inahitajika sana kwa ujumuishaji wa dijiti wa Afrika katika zama ambazo mvuto wa ujuzi wa mahali pa kazi tayari unabadilika mtandaoni.


## Sands Resources (Tanzania) Limited.

## Taarifa kwa Umma

***Novemba 26, 2020 – Dar es Salaam:***

Bodi ya wakurugenzi wa kampuni ya Sands Resources (Tanzania) Ltd inapenda kuujulisha umma kuwa imefikia uamuzi wa kufuta usajili wa kampuni hii na shughuli zake zote hapa nchini.

Kampuni hii ilisajiliwa tarehe 17 Novemba 2019 chini ya sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na BRELA, Ikiwa na lengo la kupata vitalu na kufanya shughuli za utafiti na uchimbaji wa madini ya mchanga. Hata hivyo tangu kuanzishwa kwake kampuni hii haikuwahi kufanya shughuli yoyote sawasawa na lengo lake.

Hivyo bodi ya wakurugenzi imefikia muafaka wa kufuta usajili wa kampuni hii kwa msajili wa makampuni pamoja na shughuli zote ilizokuwa inakusudia kuzifanya kupitia kampuni hii.

Kwa taarifa hii, Bodi ya Wakurugenzi ingependa kuufahamisha Umma kwamba shughuli zote ambazo zilikuwa chini ya Sands Resources (Tanzania) Limited zilikoma kuanzia tarehe 16 Novemba 2020.

Tunawashukuru sana wadau wote ambao tumekuwa tukishirikiana nao katika kipindi chote. Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa: **Simu: +255 22 260 0430**
**Email: enquiries.tanzania@strandline.com.au**


# Wadaiwa kutonyonyesha watoto wakihofia kuharibu maumbile yao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BAADHI ya kinamama mkoani Shinyanga, wamedaiwa kuendekeza imani potofu kuwa wakinyonyesha watoto wao mara kwa mara, matiti yatalala na kuharibu maumbile yao, hivyo kukosa mwonekano mzuri.

Kaimu Mratibu wa Lishe Manispaa ya Shinyanga, Loyce Nicolao, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe, kuhusu hali ya unyonyeshaji watoto, yakiwamo maziwa ya awali ya njano pale mama anapojifungua ili kumpatia mtoto kinga ya mwili.

Alisema katika utafiti walioufanya, baadhi ya kinamama hawapendi kunyonyesha watoto mara kwa mara kwa madai ya kuharibu maumbile yao. Kwa mujibu wa utafiti huo, wanawake hao wanadai kuwa kwa kufanya hivyo matiti yanawahi kulala pamoja na kudai kuwa maziwa ya awali ya njano kudai ni machafu.

Hatua hiyo, Nicolao alisema imesababisha hali ya unyonyeshaji kutokuwa ya kuridhisha katika manispaa na mkoa kwa ujumla.

"Takwimu za unyonyeshaji mwaka 2019 katika Manispaa ya Shinyanga zinaonyesha kuwa kati ya watoto 10,150 walionyonyeshwa maziwa ya mama ndani ya saa moja hadi miezi sita ni 7,713 sawa na asilimia 76 na mwaka huu, hadi Oktoba, kati ya watoto 7,657 ni 6,380 sawa na asilimia 83," alisema Nicolao.

# Baba asakwa tuhuma za mauaji ya mwanawe

**Na Richard Makore, MWANZA**

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linamsaka mkazi wa Nyamadoke Kata ya Buswelu wilayani Nyamagana, Adam Athuman, kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wake, Athumani Adam (10) aliyekuwa akisoma darasa la tatu Shule ya Msingi Nyamadoke.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 22, mwaka huu nyumbani kwa mtuhumiwa na kwamba marehemu alimshambulia mwanawe kwa fimbo katika sehemu mbalimbali za mwili wake.

Alisema mtuhumiwa alitoroka baada ya kutekeleza mauaji hayo, na kwamba wanamsaka.

Kamanda Muliro alisema mwili wa marehemu umeshafanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando na kukabidhiwa kwa familia kwa ajili ya mazishi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyamadoke Wilaya ya Ilemela, Musa Manyilizu, alisema siku ya tukio alipigiwa simu kwamba kuna mtoto amepigwa na hali yake ni mbaya.

Aliongeza kuwa alipofika eneo la tukio alikuta mtoto akiwa na hali mbaya akiwa na alama sehemu za mikono, akiwa amekatwa mdomo kwa kutumia mkasi pamoja na miguu ikiwa na alama.

Alisema baada ya kuona hali ya mtoto huyo aliamua kumbeba kwenye baiskeli yake na kumkimbiza polisi kwa ajili ya kupatiwa PF3 ili ampeleke hospitali.

HABARI KITAIFA

# Kibano watakaouza saruji zaidi ya 20,000/-

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, amepiga marufuku wafanyabiashara wa saruji kuuza bidhaa hiyo zaidi ya Sh. 20,000 kwa mfuko mmoja, na kwamba watakaoiuza zaidi ya bei hiyo wachukuliwa hatua.

Gabriel alitoa agizo hilo wakati akizungumza na wanyabiashara wa saruji katika mkoa huo, jana na kusema atakayekiuka agizo hilo atachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kufutiwa leseni ya biashara.

Alisema alifanya uchunguzi kubaini bidhaa hiyo kwa Sh. 22,000 na sehemu nyingine Sh. 23,000 kwa mfuko mmoja, na kueleza kuwa haiwezekani mwananchi wa kipato cha chini kumudu kununua kwa bei hiyo.

"Sisi tumeshakubaliana kwamba biashara iende kwa mujibu wa hali iliyokubalika kwa hiyo mtu yeyote anayetaka kupingana na serikali siyo jambo zuri wala rafiki," alisema na kuendelea:

"Na wafanyabiashara tumeongea lugha moja chini ya chama chao na umoja wao... atakayekiuka atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hata kupokonywa leseni."

Aidha, alisema ukaguzi wa bei ya saruji utakuwa endelevu kwa kuwa jukumu la serikali ni kumlinda mwananchi, ambaye ni mlaji awe ananunua bidhaa kwa bei inayokubalika.

Aliwataka wafanyabiashara ya saruji kuhakikisha wanaponunua wapokee risiti na wanapouza pia watoe risiti, na kuwataka kuwa waaminifu.

Mkurugenzi wa Kampuni ya G.Msenya Traders Co. LTD, Geofrey Msenya, alisema wafanyabiashara wa saruji Mkoa wa Geita wamekubaliana na maamuzi ya Mkuu wa Mkoa hawawezi kupingana na maamuzi ya serikali.

Msenya alisema vikwazo wanavyokutana navyo ni upatikanaji wa bidhaa hiyo kuwa mdogo, lakini mahitaji ni makubwa sana.




Mkuu wa Chuo cha Kodi (ITA), Prof. Isaya Jairo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya mahafali ya 13 ya chuo hicho, yatakayofanyika kesho. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Mawasiliano wa chuo hicho, Oliver Njunwa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



## Aomba msaada mil. 14.9/- kuwekewa mashine ya moyo

**Na Mwandishi Wetu**

JOYCE Nasolwa, mkazi wa jijini Arusha mwenye tatizo la moyo, anaomba msaada wa Sh. milioni 14.9 kwa wasamaria wema, ili aweze kuwekewa mashine ya mapigo ya moyo imsaidie katika upumuaji.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, alisema, kiasi cha fedha kinachohitajika ili awekewe mashine hiyo ni Sh. milioni 29.2 na ameshapata Sh. milioni 14.2.

"Mara ya kwanza nilipelekwa India na Wizara ya Afya mwaka 2011 na kuwekewa mashine ambayo sasa nimeambiwa imeisha muda wake na ninatakiwa kuwekewa nyingine," amesema Joyce. Alifafanua kuwa Julai mwaka huu alikwenda katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kupimwa na kuambiwa kuwa mashine hiyo imeisha muda wake, hivyo anatakiwa kuwekewa nyingine kwa gharama ya Sh. milioni 29. 2.

"Kwa sasa niko Dar es Salaam nikiendelea kutafuta msaada huo ili niweze kupata mashine hiyo, kwani ninateseka, hasa ninapotembea, siwe kutembea kwenye sehemu ya mwinuko, ninachoka sana," amesema.

Joyce amewaomba wasamaria wema ambao watakuwa tayari kumsaidia wawasiliane naye kwa namba 0754-689658, aweze kupata haraka kiasi cha fedha kilichosalia ili apate mashine hiyo.

# Tanzania kuimarisha mapato Sudan Kusini

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI kupitia Chuo cha Kodi Tanzania (ITA),inatarajia kuingia makubaliano na Sudan Kusini kuisaidia kuimarisha Mamlaka ya Mapato nchini humo.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, kuhusu mahafali ya 13 ya chuo hicho ambacho wahitimu 389 wanatarajia kutunukiwa vyeti katika ngazi ya shahada, stashahada na astashahada.

Alisema Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, anatarajia kuwa mgeni rasmi na wageni mbalimbali wakiwamo makamishna wa kodi kutoka nchi ya Sudan Kusini na Comoro. Prof. Jairo alifanunua kuwa chuo hicho kinawajengea uwezo wanafunzi kutoka nchi tofauti ikiwamo za Afrika Mashariki na mahafali hayo yatakuwa yametunuku jumla ya wahitimu 5,153 tangu kuanzishwa mwaka 2008.

"Chuo hiki kiliteuliwa na Afrika Mashariki kuwa kituo cha umahiri katika mafunzo kuhusu masuala ya ushuru, kodi na forodha. Tunaendelea na mazungumza na Sudan Kusini tunawasaidia kuimarisha mamlaka ya mapato vilevile tunaongea na mamlaka ya Comoro," alisema Prof. Jairo. Pia, alisema chuo hicho kimepeleka maombi ya mtaala mpya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili kuwa na mafunzo yanayoendana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia na kiuchumi.

"Mafunzo haya yataboresha mtaala wake wa masomo ili kukidhi mahitaji ya sera ya Tanzania ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda," alisema Prof. Jairo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# SADC yaonyesha mfano mapambano ya ukatili kijinsia

**KUANZIA** jana Novemba 25, nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zimeungana na Dunia kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia (GBV).

Maadhimisho hayo yatakayofikia kilele chake Desemba 10, mwaka huu, yana lengo la kupinga vitendo vyote vya ukatili.

Katika taarifa yake ya kuanza kwa maadhimisho hayo, Katibu Mkuu wa SADC, Lawrence Tax, amewataka wadau wa kupinga vitendo hivyo kuungana ili kuwaweka salama wanawake na watoto wasiendelee kutekeseka na majanga mawili kwa wakati mmoja likiwamo la vitendo vya ukatili wa kijinsia na ugonjwa wa Covid-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Kampeni ya kimataifa ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, inaitaka dunia kuweka mbele wito wa hatua za kumaliza kabisa vitendo hivyo vya ukatili ambavyo vinaleta utengano katika jamii na kuathiri shughuli za kiuchumi na maendeleo.

SADC inatambua ukatili wa kijinsia ni suala muhimu kulivalia njuga kutokana na mwelekeo wake wa kuathiri uchumi duniani.

Kutokana na hali hiyo, itafaki ya nchi za SADC kwenye suala la jinsia na maendeleo, inawezesha wanawake ili waweze kutokomeza kabisa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ubaguzi na kuleta usawa.

Hivi karibuni wanachama wa nchi za SADC walipitisha mkakati wa pamoja wa kikanda kupambana na GBV, na Katibu Mkuu, Tax anawezesha na kuratibu maendeleo ya utekelezaji wa mpango huo ili kutokomeza vitendo hivyo kwenye nchi za Jumuiya hiyo.

SADC imepongeza hatua zinazochukuliwa na nchi wanachama katika mapambo ya GBV kwenye nchi zao na kuendelea kusisitiza kutekeleza hatua madhubuti za kutokomeza vitendo hivyo.

Tanzania ikiwa ni moja ya nchi wanachama wa SADC imeanza kampeni ya kitaifa ya kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, inayoratibiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Asasi za kiraia kupitia Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI).

Kampeni hiyo kitaifa mwaka huu kaulimbiu yake ni "Tupinge Ukatili wa Kijinsia: Mabadiliko Yanaanza na Mimi".

Tanzania inafanya kampeni hiyo ikiwalenga mtu mmoja mmoja ili kuhakikisha kuwa kila mtu katika nafasi yake anapaza sauti na kuchukua hatua ya kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia husasan dhidi ya wanawake na watoto katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika nyumba tunazoishi, mahali pa kazi, shuleni na mahali pengine katika jamii zetu.

Vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni suala lisilokubalika kimataifa na katika jamii. Vitendo vya ubakaji, vipigo, matusi na kunyimwa haki za kumiliki mali vinarudisha nyuma jitihada za serikali katika kufikia usawa wa jinsia kwa kuwa waathirika wa ukatili hupata madhara ya kimwili, kisaikolojia na kiuchumi na kushusha hadhi na usawa wa mtu au familia inayofanyiwa ukatili.

Vyombo vya habari vina mchango mkubwa katika kubadilisha mtazamo wa wale wanaotenda vitendo hivyo na pia kuibadilisha jamii kwa njia mbalimbali kama mitandao ya kijamii, redio, majarida na televisheni ili kufikia malengo yake.

Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuzuia na kutokomeza ukatili huo kwa kuandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 - 2021/22). Mpango huu unalenga kupunguza kiwango cha ukatili katika jamii kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

Pia, kuandaliwa kwa Mwongozo wa kuanzisha madawati ya jinsia katika vyuo vikuu na vyuo vya kati. Hatua hizi ni kati ya nyingi ambazo serikali imechukua kuhakikisha vitendo hivi vinatokomezwa.

Ni wajibu wa kila mtu sasa kuchukua hatua ili vitendo hivi vitokomezwe kabisa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hiki ndicho kiasi cha nyama nyekundu tunachopaswa kula

Na Sabato Kasika

**KWA** muda mrefu, kumekuwapo na mjadala kutoka kwa watu wa kada mbalimbali unaohusu faida na madhara ya ulaji nyama nyekundu, ambayo ninaamini Watanzania wengi ni watumiaji.

Hiyo nyama nyekundu, ni ile yenye rangi nyekundu kabla ya kupikwa. Hapo kuna wanyama kama nguruwe, ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine, wote wanatembea kwa kutumia miguu minne.

Wapo wanaoshauri nyama hiyo iachwe na badala yake watu watumie mboga za majani na matunda kwa ajili ya kuendelea kulinda afya zao, ili kuepuka maradhi yatokanayo na ulaji wa nyama hiyo.

Mboga zinazoshauriwa kuliwa ni kama dengu, njugu na vyakula vyenye protini ya mimea ikiwamo mikate ya ngano isiyokobolewa, nafaka zisizokobolewa, karanga, maharage ya soya, kunde na vingine vingi.

Pamoja na hayo, inashauriwa kuwa mtu anatakiwa kula gramu 14 tu ya nyama nyekundu kwa siku, gramu 29 ya vyakula vitokanavyo na kuku, na gramu 13 ya mayai ama yai moja na nusu kwa wiki.

Kwamba, kwa kutumia kiasi hicho cha nyama nyekundu na kuendelea kula vyakula vya mboga, itasaidia kumuepusha mtu na maradhi yanatokana na nyama hiyo, na hivyo kuwa salama zaidi.

Ushauri huo umo katika utafiti uliochapishwa kwenye Jarida la Sayansi la Lancet mwaka jana, kuhusu mabadiliko yanayohitajika kwenye uzalishaji na ulaji wa chakula ili kuepusha vifo vya mamilioni ya watu.

Utafiti huo ulitangazwa na redio moja ya kimataifa, kwamba ni muhimu kufanya mabadiliko katika lishe ili kupunguza ulaji wa nyama hiyo na kugeukia zaidi vyakula vya mboga kwa usalama wa afya ya binadamu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, nyama nyekundu huchangia hatari kwa mtu kupata ugonjwa wa moyo na saratani ya tumbo, kwa kuwa baadhi ya nyama hiyo huwa na kiwango kikubwa mafuta.

Mafuta hayo yanatajwa kuongeza lehemu mwilini, na kwamba mtu mwenye kiwango kikubwa cha lehemu, huwa hatarini kupatwa na ugonjwa wa moyo, hivyo ni muhimu kuwa makini katika ulaji wa nyama hiyo.

Vilevile, inaelezwa kuwa nyama nyekundu ina kemikali iitwayo 'carnitine' inayofanya mishipa ya damu kukakamaa na kusababisha kuzeeka kwa ngozi. Hivyo, inajenga maana ya umuhimu na kuwapo msisitizo wa kupunguza ulaji wa nyama aina hiyo.

Pia, Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) katika taarifa yake, inasema nyama ya nguruwe inaongoza kuliwa kwa wingi duniani kwa asilimia 36, ikifuatiwa na kuku asilimia 35 na nyama ya ng'ombe asilimia 22.

Kwa kuwa nyama ya nguruwe nayo ni nyekundu na nyingine za aina hiyo, umefika wakati watu kuangalia uwezekano wa kuangukia ulaji wa kuku na kushusha nyama zote nyekundu kwa ajili ya kulinda afya.

Ni kweli, miili yetu inahitaji protini kwa ajili ya kujijengea kinga ya mwili kuanzia nyama, samaki, kuku, kunde, maziwa na vingine, lakini wataalamu wa afya wanasema, inawezekana mtu akapata kinga bila kula nyama.

Kwa hali hiyo, bado kuna haja ya kubadili mfumo wa ulaji kwa kuzingatia kile kinachoelekezwa na wataalamu hao, ikiwamo kuachana na nyama hiyo, ama kula kiasi kidogo wanachoshauri.

Inawezekana watu wengi wamekuwa wakikutana na utata kuhusu nyama nyekundu, lakini ni vyema kuzingatia maelekezo ya wataalamu ili kuendelea kulinda afya kuliko kubaki kwenye mashaka.

Utata huo unakuwapo kutokana na maelezo mbalimbali yakiwamo kwamba, mtu anatakiwa kuchagua nyama ya ng'ombe anayepelekwa malishoni kula nyasi, na si anayelishwa mashudu ya mahindi ama nafaka mbalimbali.

Kwamba, kuna tofauti kubwa kati ya ng'ombe anayechunga nyasi na yule anayelishwa kwa kufugwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa, kwa kuwa nyama yake si salama, kama ilivyo ya yule anayepelekwa malishoni kula nyasi.

Jambo muhimu ni katika kulinda afya, hivyo kila Mtanzania hana budi kutafakari kwa kina kuhusu ulaji nyama nyekundu na kisha kuchukua hatua sahihi za kunusuru afya yake.

HABARI PICHANI

# Makamu wa Rais wa GGM atembelea IPP Media



Makamu wa Rais wa Geita Gold Mine, Simon Shayo, akiagana na viongozi wa The Guardian Ltd.



Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa GGM, Stephen Mhando (kulia), akitaka ufafanuzi wa jinsi ya uendeshaji wa vipindi vya East Africa Radio/ Televisheni walipotembelea chumba cha habari. Wapili kushoto ni Makamu wa Rais wa GGM, Simon Shayo.



Makamu wa Rais wa Geita Gold Mine, Simon Shayo, akizungumza baada ya kutembelea vyombo vya habari vya IPP jijini Dar es Salaam jana.



Makamu wa Rais wa Geita Gold Mine, Simon Shayo (kulia), akiwa katika studio ya kurushia taarifa ya habari ya ITV. Kushoto ni Mkurugenzi wa Vipindi, Koigi Mcharia na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa GGM, Stephen Mhando (katikati).



Meneja wa Kiwanda cha Uchapaji Magazeti cha The Guardian Ltd, Balasubramaniyan Venkadachalam, akifafanua jinsi ya uchapaji wa gazeti.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, akieleza jinsi chumba cha habari kinavyofanya kazi kwa Makamu wa Rais wa GGM, Simon Shayo na ujumbe wake. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**

# Wizara yaanza kupanga ardhi Chamwino

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeanza kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika vitongoji 14 vilivyoko katika Kata ya Chamwino mkoani Dodoma.

Kazi hiyo ilianza juzi kwa timu kutoka wizarani chini ya Mkurugenzi Msaidizi wa Upimaji na Ramani, Elizabeth Mrema, kukutana na wananchi wa vitongoji hivyo ili kuangalia namna bora ya kuendeshaji mpango huo.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Usanifu Miji na Mipango Kabambe, Immaculate Senje, aliwataka wananchi wa vitongoji vya Chamwino kuhakikisha wanamaliza tofauti za migogoro midogo midogo ya ardhi katika maeneo yao kabla ya wataalamu hawajafika uwanjani kurahisisha kazi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi.

Alisema iwapo wananchi wa maeneo husika watashindwa kumaliza tofauti zao za migogoro ya ardhi mapema, wataalamu watakapofika watashindwa kuendelea na kazi hiyo mpaka utatuzi wa mgogoro ukapomalizika.

"Zoezi (kazi) la (ya) upimaji katika eneo la Chamwino hapa Dodoma linalenga (inalenga) pia kupata maeneo ya miundombinu ikiwamo barabara na itazingatia njia za awali na kuepuka kugusa nyumba za wananchi," alisema Senje.

Naye Mrema aliwatoa hofu wananchi wa maeneo hayo kuhusiana na kazi hiyo na kuwataka kuwapa ushirikiano wataalamu wa wizara watakaokuwa wakifanya kazi hiyo.

Alisema hofu ya wananchi kuwa wanaweza kudhulumiwa maeneo yao kupitia kazi hiyo si ya kweli na kusisitiza kuwa wizara imeamua kuboresha vitongoji vya kata ya Chamwino ili kuwawezesha wananchi kuwa na nyaraka za umiliki wa maeneo yao.


Kwa mujibu wa Mrema, kazi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi Chamwino itaanza na vitongoji vitano na baadaye kuendelea na vitongoji vingine hadi kufikia 14.

Alivitaja vitongoji vitano ambavyo zoezi hilo litaanza kuwa ni Sokoine, Ukombozi, Kambarage, Umoja na Azimio.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Letare Shoo, aliwaambia wananchi wa Chamwino katika mkutano huo kuwa kazi ya upangaji, upimaji na umilikishaji maeneo imegawanyika katika makundi makuu mawili.

Aliyataja makundi hayo kuwa ni urasimishaji au uboreshaji maeneo yaliyojengwa bila kufuata taratibu na kupima mashamba makubwa kwa kuainisha matumizi yake ikiwamo viwanja.

Hata hivyo, ofisa huyo alisema tofauti na maeneo mengine, wananchi wa Chamwino watapata unafuu katika gharama wakati wa utekelezaji wa kazi hiyo na kwamba badala ya kulipia Sh. 150,000 watalipia Sh. 50,000 kwa kila kiwanja.



Mmoja wa wateja wa Zantel, Edward Julius Kabuyu, akipewa huduma katika duka jipya la Zantel, lililozinduliwa mjini Wete, Pemba juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC akunwa na kasi ujenzi hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, ameridhishwa na hatua ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ubungo na kumwelekeza mkandarasi, SUMA JKT, kuhakikisha kazi hiyo inakamilika na kukabidhiwa kabla ya Januari 8, mwakani.

Kunenge alitoa maelekezo hayo juzi alipotembelea kukagua kazi hiyo na kujionea majengo sita kati ya saba yakiwa katika hatua ya upauaji. Kwa mujibu wa mkandarasi, ujenzi huo umefikia asilimia 60.

Mkuu huyo wa mkoa alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuridhia kutoa fedha za ujenzi huo, ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi wa Ubungo ambao kwa muda mrefu walikuwa wakisafiri hadi Sinza kufuata huduma.

Pia aliipongeza SUMA JKT kwa kazi nzuri inayoifanya pamoja na uongozi wa wilaya katika kusimamia mradi huo.

Naye Mkurugenzo wa Viwanda wa SUMA JKT, Luteni Kanali Edward Antony, alimhakikishia Kunenge kuwa ujenzi huo utakamilika na kukabidhiwa ndani ya wakati.

Katika hatua nyingine, Kunenge aliwahakikishia wakazi wa Kifuru na Chanika kuanza kupata huduma za maji safi ifikapo Desemba 31, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyotoa Rais Magufuli wakati wa mkutano wa kampeni jijini humo.

Kunenge aliongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na watendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo na kushuhudia mradi wa ujenzi wa tangi la maji lenye uwezo wa kupokea lita milioni mbili kwa siku likiwa limekamilika kwa asilimia 100.

Tangi hilo litakuwa likipokea maji kutoka Kisarawe na kutawanya kwa wananchi wa Kifuru, Chanika, Banana, Gongo la Mboto na Pugu.

Aidha, Kunenge alionyesha kuridhishwa na hatua ya ujenzi uliopofikia. Hadi sasa DAWASA imelaza mabomba kutoka Kisarawe hadi Pugu urefu wa kilomita 4.5 na kazi iliyobaki ni kulaza mabomba kutoka tangi lilipo na kuyatawanya kwa wananchi.

Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema kwa sasa wafanyakazi wanaendelea na kazi ya kuhakikisha ifikapo Desemba 31, maagizo yote ya Rais Magufuli yametekelezwa kwa vitendo.

## Wahitimu wa kike waongezeka Mzumbe

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

IDADI ya wahitimu wa kike katika Chuo Kikuu Mzumbe imeongezeka na kufikia asilimia 50.5, huku wanaume wakiwa asilimia 49.5 baada ya jamii kuanza kuelewa umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Lugano Kusiluka, alisema hayo juzi kwenye mahafali ya 19 yaliyofanyika Kampasi Kuu ya Chuo hicho, mje kidogo ya mji wa Morogoro.

Prof. Kusiluka alisema sababu ya ongezeko hilo inatokana na kuwekewa mazingira mazuri ya masomo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya hosteli. Alitaja sababu nyingine kuwa ni familia nyingi nchini kuanza kutambua umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike.

Alisema awali kuenea kwa mfume dume na ukatili wa kijinsia vilivyokuwa vikiendelezwa na baadhi ya familia kutokana na utamaduni potofu, vilichangia mtoto wa kike kushindwa kupelekwa shuleni.

Kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chuoni hapo, Prof. Kusiluka alisema serikali imekuwa ikiendelea kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia ili kuongeza wanafunzi wa kike na hatimaye kuongeza viongozi wanawake.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano, serikali imetoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu mbalimbali chuoni hapo ikiwamo ujenzi wa mabweni, hosteli na miundombinu mifumo ya maji na barabara.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Prof. Matthew Luhanga, alisema pamoja na kuwa miongoni mwa vyuo vikuu vikongwe nchini, wanachojivunia ni kuwapo ongezeko kubwa la wanafunzi wa kike wanaohitimu elimu ya juu kwa fani mbalimbali chuoni hapo.



Nyasi zikiwa zimeota kwenye mtaro katika Barabara ya Sewa, eneo la Mikocheni Viwandani, jijini Dar es Salaam, kitendo kinachosababisha maji kushindwa kupita nyakati za mvua. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima wa viazi lishe walia na masoko ya nje

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

WAKULIMA wa viazi lishe katika Kijiji cha Negezi, Kishapu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuwatafutia masoko ya nje ili kuongeza kasi ya uzalishaji na kuendelea kupungua wimbi la utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano.

Waliyabainisha hayo juzi wakati wakizungumza na gazeti hili baada ya kukagua mashamba ya viazi lishe, utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma za lishe katika kuimarisha afya ya mama na mtoto (ENRICH) unaotekelezwa na halmashauri tano za mikoa ya Shinyanga na Singida chini ya World Vision Tanzania.

Dogani Mwanzalima, mmoja wa wakulima hao, alisema baada ya kupewa elimu ya kilimo cha viazi lishe na World Vision anazalisha viazi lishe kwa wingi na kukosa masoko ya uhakika licha ya sehemu yake kutumia nyumbani kuimarisha afya za watoto.

Alisema msimu uliopita wa mwaka 2019 alilima matuta 25 na kupata tani nne za viazi lishe na kutafutiwa masoko na World Vision Tanzania katika kiwanda cha kuongeza thamani viazi lishe Maswa na kupata Sh. milioni 1.7.

"Mimi nilikuwa sina mwamko wa kulima viazi lishe. Nilihamasishwa kulima zao hili na wake zangu waliokuwa wakipatiwa mafunzo kutoka World Vision. Nilitafutiwa masoko katika kiwanda cha lishe Maswa.

"Baada ya kuuza viazi hivi nilipata Sh. milioni 1.76 na tukapanga na wake zangu tukanunua ng'ombe wawili wa kilimo kila mmoja Sh. 500,000 na ng'ombe mmoja wa maziwa kwa Sh. 380,000 kwa ajili ya maziwa ya watoto ili kuendelea kuimarisha afya zao. Naye Veronica Amos alisema wamekuwa wakizalisha viazi lishe na kuuza kilo moja kwa Sh. 6,500 daraja la kwanza na Sh. 3,000 daraja la pili kwa kilo katika kiwanda cha Maswa na kuomba serikali kuwatafutia masoko ya nje, ili kuongeza ushindani wa masoko.

Alisema kuwa na masoko ya nje kutawezesha wakulima kunufaika na kilimo cha viazi lishe kama ilivyo kwenye mazao mengine ya kimkakati kama vile pamba, tumbaku na ufuta na kwamba itasaidia kutoendelea kutegemea kiwanda kimoja tu.

Mratibu wa ENRICH, Dk. Frank Mtimbwa, alisema wamewapatia elimu wananchi 112 kutoka Kishapu, Kahama na Shinyanga namna ya kulima na kuhifadhi viazi lishe lengo likiwa familia kulima na kutumia viazi hivyo.

Alisema World Vision kwa kushirikiana na serikali walianzisha kiwanda cha kuongeza thamani ya viazi lishe kama njia ya kuwatafutia masoko wakulima na kuongeza uzalishaji na kwamba viazi hivyo kwa sasa vinaliwa zaidi katika mikoa ya Simiyu, Tabora na Geita.

# Afariki dunia kwa ajali ya pikipiki

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa Nakayaya, Tunduru mkoani Ruvuma, Hashim Mtuichi (19) amefariki dunia baada ya pikipiki aliyokuwa akisafiria kuanguka.

Pia katika ajali hiyo, vijana watatu aliokuwa amewabeba katika pikipiki hiyo, wamenusurika kifo na kulazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru kwa matibabu.

Walionusurika katika ajali hiyo iliyotokea juzi na kulazwa wametajwa kuwa ni Yusuph Mkanga (19), Shukuru Seif (19) na Omari Seif (18) ambao alikuwa amewabeba 'mshikaki'.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema chanzo cha ajali hiyo ambayo ilitokea katika makutano ya barabara ya Tunduru Masasi na Tunduru kwenda Bomani ni mwendokasi wa dereva, hivyo kumfanya ashindwe kuimudu pikipiki yake. Walisema ajali hiyo ambayo ilisababishwa na pikipiki aina ya SLG yenye namba za usajili MC 606 CGV, kugonga kizingiti cha barabara.

Kwa mujibu wa mashuhuda hao, ajali hiyo ilitokea majira ya saa 4.30 usiku wa kuamkia juzi na kwamba baada ya tukio hilo, wasamaria wema walijitokeza na kuwasaidia kuwapeleka hospitalini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amedhibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba polisi wanaendelea na uchunguzi ili kujua chanzo chake.

Kutokana na ajali hiyo, Kamanda Maigwa aliwasisitiza madereva wanaoendesha vyombo vya moto kuzingatia usalama wa maisha yao na waenda kwa miguu pindi wanapokuwa wakiviendesha ili kuokoa maisha yao na ya watu wengine.

# Wafanyabiashara wakubali kutokupandisha bei ya saruji

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

UONGOZI wa Mkoa wa Tabora umekutana na wafanyabiashara wa vifaa vya ujenzi na saruji na kukubaliana faida wanayopata katika kila mfuko wanaouza isizidi Sh. 500, ili kutowaumiza wananchi.

Uamuzi huo ulifikiwa juzi katika mkutano ambao uliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, kwa lengo la kutafuta mwafaka wa kutatua tatizo la bei ya saruji kupanda.

Akifungua mkutano huo, Dk. Sengati alisema serikali haikusudii kuwapangia bei elekezi, lakini wafanyabiashara wanalo jukumu la kuuza bidhaa hiyo kwa bei ambayo haitawafanya wananchi washindwe kujenga na kuishi katika nyumba bora.

Dk. Sengati alisema kimsingi hakuna sababu zinazoweza kuhalalisha wafanyabiashara kupandisha saruji na kwamba wako wanaouza Sh. 23,000 hadi 30,000 kwa mfuko mmoja wakati wananunua kiwandani kwa Sh. 11,000 hadi 13,000.

Alisema gharama za usafirishaji na posho za vibarua na madereva haiwezi kufanya bei ipande kwa kiasi hicho ambacho inawaumiza wananchi.

Dk. Sengati alisema pamoja na kuwa si jukumu lake la kupanga bei, serikali ina wajibu wa kuhakikisha bei za bidhaa zilizoko sokoni haziwaumizi wananchi na kuwafanya wachukie serikali yao.

Alisema wafanyabiashara ni wadau muhimu katika kushirikiana na serikali kwenye shughuli za maendeleo, hivyo ni vyema wakahakikisha saruji inauzwa kwa bei nafuu ambayo haiwaumizi wananchi.

"Tumebaini wafanyabiashara wa rejareja wanauza saruji kwa Sh. 23,000 hadi 30,000 wakati bidhaa hizo amechukulia hapa hapa Tabora na hana gharama kubwa za kusafirisha mizigo. Kitendo hicho ni kutaka kutengeneza fedha nyingi kwa kuwaumiza wanyonge na hakikubaliki. Serikali haiwezi kuvumilia, tutawachukulia hatua," alisema.

Pia alisema wafanyabiashara wanatakiwa kuwa wazalendo kwa kuungana na maono na mtazamo wa serikali ambao unataka ubora na unafuu wa maisha kwa wananchi.

Mmiliki wa Kampuni ya Vimajo and Sons, ambaye ni miongoni wa wafanyabiashara wakubwa wa saruji mkoani hapa, Victor Chami, alisema hivi sasa saruji inapatikana kwa shida na wakati mwingine wanalazimika kununua kwa wafan-

# Miaka 5 jela kumgonga mwendesha pikipiki

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita, imemhukumu Irene Boazi (23), mkazi wa Nyankumbu, kutumikia kifungo cha miaka mitano jela au kulipa faini ya Sh. 120,000 na fidia ya Sh. 500,000 kwa kukutwa na hatia ya kumgonga mwendesha pikipiki na uharibifu wa chombo hicho.

Mlalamikaji ambaye ni askari wa Jeshi la Magereza, Abas Selemani, katika ajali hiyo alivunjika mguu na pikipiki yake kuharibiwa.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alilipa faini ya Sh. 120,000 na kuachiwa huru na fidia ya mlalamikaji Sh. 500,000 kwa ajili ya matibabu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Samwel Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Clemence Kato, ulipeleka mahakamani mashahidi wanne na vielelezo vinne ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo.

Hakimu Maweda alisema mshtakiwa alikuwa akiendesha gari aina ya Daihatsu yenye namba za usajili T 558 CVX, akitokea Geita mjini kuelekea Nyankumbu akiwa kwenye mwendo wa kasi na alipofika mbugani maeneo ya matuta alihama na kwenda kulia nje ya barabara na kumgonga Selemani ambaye alivunjika mguu wake wa kulia mara mbili pamoja na uharibifu wa pikipiki.

Hakimu Maweda alisema katika kutathimini ushahidi wa pande zote, upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote mawili kwa kutumia mashahidi wawili.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella (kulia), akipokea msaada wa kompyuta mbili zenye thamani ya Sh. milioni 3.5 kutoka kwa Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Posta (TPB), Regina Semakafu, kwa ajili ya ofisi ya ardhi ya mkoa huo, jana. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

# CCM yawaonya madiwani kuhusu makundi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, kimewaonya madiwani wanaoendekeza makundi na kuwataka kuacha mara moja.

Pia wametakiwa kuelekeza nguvu zao na kuungana ili kusimamia miradi ya maendeleo inayoletwa na serikali kwenye maeneo yao.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, Edward Mmavele, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na madiwani katika kikao cha uchaguzi wa wenyeviti wa Halmashauri ya Mji wa Masasi na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, uliofanyika katika ukumbi wa CCM wilayani hapa.

Mmavele alisema kuna baadhi ya madiwani wa chama hicho bado wanaendeleza makundi ambayo yalijitokeza katika uchaguzi uliomalizika oktoba 28, mwaka huu, na kwamba makundi hayo hayana tija kwa sasa na yanapaswa kuvunjwa mara moja.

Alisema kuendekeza makundi ndani ya chama ni hatari na kunalenga kukichafua chama ikiwa ni pamoja na kuzorotesha jitahada kutekeleza ilani ya uchaguzi na miradi ya maendeleo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, sasa ni wakati mwafaka wa kuvunja makundi yote ndani ya chama na kuungana ili kukipigania chama katika kusimamia maendeleo ambayo yanalenga kuwahudumia wananchi.

Mmavele alisema kila diwani aliyepita katika eneo lake, wananchi wamempa ridhaa na kumwamini kuwa ana uwezo wa kuwasemea matatizo yao na kuwaletea maendeleo na si kwenda kujiunga katika makundi ya kujengeana chuki na uhasama.

"Naomba tuyavunje makundi kwani uchaguzi umeshapita. Hakuna sababu ya kuendeleza makundi miongoni mwetu bali turudi pamoja na tufanye kazi ili tukijenge chama na tuwahudumie wananchi wetu," alisema Mmavele. Kuendeleza makundi, alisema ni kujiweka katika hatari ya kupoteza nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa mwaka 2025 kwa vile uwapo wa makundi huenda yakadumu mpaka uchaguzi ujao.

Mmavele alisema hatari kubwa ya kuwa na makundi ni pamoja na kushindwa kufanya vikao halali vya chama hasa katika ngazi ya vijiji.

Naye Ibrahim Chiputula, Mwenyekiti mpya wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, alisema ushirikiano ni jambo jema kuliko kuwa na makundi yasio na tija ambayo yatasababisha dosari ndani ya chama.

# Serikali yasisitiza kutoruhusu matumizi ya GMO

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesisitiza kuwa haijaruhusu matumizi ya mbegu zilizobadilishwa vinasaba (GMO) kwa ajili ya uzalishaji na zilizopo nchini zipo kwa ajili ya utafiti peke yake.

Msisitizo huo ulitolewa juzi na Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Joseph Sokoine, wakati akifungua kongamano la wazi la kujadili usalama wa mbegu lililoandaliwa kati ya Taasisi Mwamvuli ya Kilimo Hai Tanzania (TOAM) na shirika linalojishughulisha na baionuwai (TABIO) na kuhusisha wadau wa kilimo.

Sokoine alisema kumekuwapo na maneno kuwa mbegu za GMO zinatumika wakati si kweli.

"Tuna mashamba kwa ajili ya utafiti wa mbegu hizi za GMO mfano kule Makutopola Dodoma, hatuzalisha ila zipo kwa ajili ya utafiti, serikali lazima tujiridhishe kabla ya kuruhusu kutumika au kutotumika," alisema Sokoine.

Alisema ipo sera ambayo inatambua teknolojia inayoleta maendeleo kwenye kilimo, lakini sera inayotambua kilimo endelevu.

"Mijadala kama hii juu ya usalama wa mbegu itasaidia kwa kiasi kikubwa kuona njia sahihi ya kuifuata katika utunzaji na uwendelezaji wa mbegu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho, niipongeze TOAM na TABIO kwa kuleta huu mjadala," alisema.

Mkurugenzi msaidizi wa maendeleo ya mazao katika Wizara ya Kilimo, Beatus Malema, alisema serikali inaunga mkono kilimo endelevu (kilimo hai), na kuwataka watu kuwekeza kwenye pembejeo.

"Tunaamini kilimo hai kinatunza ardhi yetu kutokana na kutokuwapo kwa matumizi ya kemikali, watu wanaweza wakawekeza kwenye kilimo hiki hususani kwenye eneo la pembejeo kama mbolea za asili na dawa za kuua wadudu za asili," alisema.

Alisema wanatambua mbegu za asili ndizo chanzo cha mbegu zote zikiwamo zinazobadilishwa vinasaba, hivyo kuna haja kubwa ya kuzitunza kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TOAM, Dk. Mwatima Abdallah Juma, alisema duniani kwa sasa kuna msukumo mkubwa wa matumizi ya GMO, hali inayohatarisha usalama wa mbegu za asili.

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI NOVEMBA 26, 2020



Ukurasa 12

**Kusambazwa umeme kunavyookoa uhai katika vituo vya afya Kigoma**



Ukurasa 14

**Uswisi wajiunga mradi shirikishi unaosimamia ustawi msitu vijijini**

## UTAFITI TAASISI YA MOYO....

# Unene; janga linaloiteka jiji Dar na simulizi 'bonge' wa kilo 160

**Na Christina Mwakangale**

KWA jamii za Kiafrika, mtu anapozungumzia unene, fikra ya kwanza inayomjia ni katika sura ya mafanikio.`

Pia, nchini kuna dhana kutoka baadhi ya makabila kutambua mwenye hali hiyo, amefanikiwa kwa ngazi muhimu kwa maisha ya uchumi.

Takwimu rasmi za kiafya zinaitaja Dar es Salaam kuongoza kuwa na watu wanene wengi, vitambi vitokanavyo na kutumia vyakula visivyowafaa, hata kuhatarisha maisha yao, ikiwamo kupata magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), umebaini watu 4,461 kati ya 6,691 sawa na theluthi mbili, waliofanyiwa utafiti jijini Dar es Salaam mwaka huu wana uzito uliopindukia.

Tabibu bingwa wa magonjwa ya moyo na Mkuu wa Idara ya Utafiti na Mafunzo wa taasisi hiyo, Dk. Pedro Pallangyo, ameiambia Nipashe kuwa utafiti wao umebaini hayo na visababishi vyake.

"Ulimwenguni kote, kuna mabadiliko ya ongezeko la magonjwa na idadi ya watu na kusababisha kukua kwa matumizi ya lishe ya bidhaa zenye 'energy' (nishati) kubwa ya chakula na hasa wanga," anasema Dk. Pallangyo.

Athari zake, ni uzito mkubwa kiafya unaochangia uwezekano wa mtu kupata magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, saratani na magonjwa ya moyo kushindwa kufanya kazi, hata kuishia vifo vya ghafla."



Musa Mkunda, akizungumza na Nipashe wodini alikolazwa MNH, mwishoni mwa wiki. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**

Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia takwimu zake za mwaka 2016, linasema unene uliopitiliza, unahatarisha afya na kuna watu wazima bilioni 1.9 duniani wanaokabiliwa nalo.

Pia, WHO inakadiria unene kupindukia umechangia watu milioni nne duniani kufariki dunia mwaka 2017, ikiwa ni ongezeko mara tatu, kulinganisha na mwaka 1975.

Dk. Galbert Fedjo, Mwakilishi wa WHO nchini, akizungumza katika wiki ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, anasema ni tatizo sasa duniani kote.

Rekodi iliyopo, magonjwa hayo yanachangia vifo milioni 41, sawa na asilimia 72 ya vifo vyote milioni 47 vilivyotokea mwaka 2018, kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2018.

### UTAFITI JKCI

Utafiti wa Taasisi ya Moyo uliofanyika jiji Dar es Salaam, kati ya Julai, 2018 hadi Agosti, mwaka jana, katika ripoti iliyoitoa Septemba, mwaka huu, ulihusisha washiriki tofauti.

Dk. Pallangyo anasema, uchunguzi uliofanywa na wataalamu bingwa, theluthi mbili walithibitika ni wazito kupindukia.

"Huu ni utafiti mkubwa kuliko yote iliyowahi kufanyika kwenye jamii yetu. Ulilenga kupima ukubwa wa tatizo la uzito mkubwa na visababishi vyake. Tulipima watu 6,691 na tukagundua zaidi ya theluthi mbili walikuwa na uzito mkubwa kupindukia," anasema.

Vyanzo hatari anataja kuwa vyakula vilivyofungashwa, upombe, kutokuwa na utaratibu unaoeleweka wa kifungua kinywa, unywaji hafifu wa maji na matumizi zaidi ya soda, matumizi madogo ya mboga za majani na matunda.

Dk. Pallangyo anasema, kwa ujumla wanawake walikuwa na uzito mkubwa kuliko wanaume, hasa kwa wenye umri unaozidi miaka 40.

### SABABU HIZO

Dk. Pallangyo anasema, utatiti uliwalenga wakazi wa Dar es Salaam, tathmini ikiwaangukia watumiaji vinywaji laini viwandani,

Endelea Uk. 12

AFYA

Inatoka Uk. 11

# Unene; janga linaloiteka jiji Dar na simulizi 'bonge' wa kilo 160

watumiaji vilevi na uvutaji sigara.

Matokeo yanaonyesha chanzo ni lishe duni, kutofanya mazoezi, husan kwa wakazi waishio mijini, tatizo linalotajwa wanalo theluthi tatu ya wakazi duniani, huku Kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika (SSA) kunashuhudiwa ongezeko la uzito huo.

"Kati ya walio na umri wa miaka zaidi ya 40, wanaume walikuwa asilimia 54.2 ya wote waliofanyiwa utafiti; theluthi mbili walikuwa watumiaji wa vilevi; na asilimia 6.9 na wana historia ya kuvuta sigara.

"Asilimia 88.3 ya washiriki wote walikuwa hawafanyi mazoezi; asilimia 4.7 wana historia ya kisukari; na asilimia 18.1 waligundulika kuwa na shinikizo la damu," anabainisha Dk. Pallangayo.

Bingwa huyo anasema, uzito kupindukia ulibainika kwa asilimia 34.8 na unene asilimia 32.4 ya washiriki hao, huku wanawake walio na umri zaidi ya miaka 40 wakiwa na tabia za kutokunywa kifungua kinywa.

**MADHARA**

Utafiti unaeleza uzito na unene kupindukia, unahatarisha afya ya moyo, ikichangia asilimia 14 ya madhara yote.

Pia unene unatajwa kuchangia kisukari kwa asilimia 44; shinikizo la damu kwa asilimia 70; na asilimia 41 inaangukia maradhi saratani.

Hadi sasa inatajwa uchumi wa dunia unaathiriwa sana na matatizo ya uzito wa binadamu, ikigharimu matumizi ya takribani Dola za Marekani trilioni mbili kutibu kila mwaka, waathirika wakubwa ni nchi zenye uchumi mdogo na kati.

**MAADHIMISHO KUDHIBITI**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, katika kilele cha Maadhimisho Wiki ya Magonjwa Yasiyoambukiza Novemba 16, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, alisema maradhi hayo kwa kipindi kati ya mwaka 2011 hadi 2025, zinatarajiwa zitakuwa zimetumia wastani wa Dola za Marekani trilioni saba.

Ni maadhimisho yaliyofanywa na hospitali, pia taasisi zinazoshughulika na afya mkoani Dar es Salaam na mkuu wa mkoa ana hoja zaidi, anayotamka:

"Gharama za huduma ya magonjwa yasiyoambukiza itafikia asilimia 75 ya bajeti ya afya duniani. Ugonjwa wa Kisukari pekee gharama zake ni Dola za Kimarekani bilioni 465 sawa na asilimia 11 ya bajeti ya afya duniani."

**SHIDA YA MLO**

Ofisa Lishe kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila Theresia Thomas, anasema athari za ulaji wanga zinachangia unene na uzito uliopitiliza.

"Kitu kinachosababisha uzito mkubwa ni vyakula vya wanga. Hii inatokana na maisha yetu tunategemea chakula hicho, tunafikiri vyakula vyenye protini ni gharama," anasema.

Anasema, ingawa kuna wanaopinga ulaji mboga za ziada wakidai sio lishe, lakini ukweli matumizi yake ni hitaji muhimu mwilini, ilhali ziada ya wanga inawaongezea matiti, makalio na vitambi, kwa sababu unajihifadhi kwenye maeneo hayo mwilini.

Theresia anaeleza hatua wanazozifanya ni kuwapa elimu ya udhibiti kwa wenye magonjwa kama presha na kisukari kuhusu lishe hospitalini hapo.

**KISUKARI?**

Bingwa wa Kisukari kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Wolfgang Bernard, anasema kiafya kila mtu anatakiwa kula chakula kulingana na kazi anayoifanya na kuzingatia lishe.

Anasema ulaji unaozingatia lishe bora, imo katika ushauri muhimu wa kiafya kutoka kwa wanasayansi, vyanzo vingi vya maradhi hutoka kwenye ulaji mbaya.

"Chakula cha wanga kwa wingi huchosha kongosho na kufanya utendaji kazi wake kuwa mkubwa na kulichosha na baada ya muda mfupi husababisha 'insulini' kupungua mwilini," anaeleza Dk. Bernard.

Anasema kisukari imeshawakumba Watanzania milioni 1.2, akitaja dalili zake mtu anakosa sukari mwilini na uwezo wa kutengeneza insulin, ikiwa na uwezo wa chini wa kufanya kazi yake kwenda kwenye misuli ya damu.

"Ushahidi wa kitabibu umebaini ongezeko hilo halikuwepo miaka ya nyuma. Kutokana na mabadiliko ya mtindo wa maisha, zamani watu walifanya kazi zaidi za kutembea, kazi za mikono na kujishughulisha muda wote, kuwafanya kuwa na nguvu."

Dk. Bernard anawashauri wanaofanya kazi ofisini kuepuka ulaji vyakula vya wanga na sukari, badala yake wawaachie wanaofanya kazi ngumu.

"Ni muhimu kufanya mazoezi kwani hufanya mzunguko wa damu mwili mzima na 'calories' nyingi kuchomwa.

"Kupunguza vyakula vyenye 'carbohydrate' (wanga), watu wale mlo ambao una nafaka ambazo hazijakobolewa, mbogamboga na matunda," anasema bingwa huyo.

**WADAU & WIZARA**

Mwenyekiti wa Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Dk. Andrew Swai, anaeleza umuhimu wa kutolewa elimu kuhusu magonjwa hayo na jamii ibadili mfumo wa maisha, ukiendana na ufanyaji mazoezi.

Mkurugenzi wa Idara ya Tiba katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Maghembe, anakiri ukubwa wa tatizo na serikali inachukua hatua kutatua matatizo ya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa yanayowakabili wananchi wengi sasa, shida kuu ni uelewa mdogo.



Mtafiti bingwa, Dk. Pedro Pallangyo. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Hapa nilipo siwezi kupata kazi wakikataa nikienda kuomba kazi katika usafiri wa daladala inabidi siti ya watu wawili nikae peke yangu," anasema.**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), katika ripoti yake mwaka 2013, inaonyesha maradhi yasiyo tya kuambukiza huathiri nyanja zingine za kijamii, huku kukiwapo ubashiri ifikapo mwaka 2033 gharama za kuhudumia itafika Dola za Marekani Trilioni 47.

UNDP inafananisha, kuwa fedha hizo zingeweza kutumika kupunguza umasikini kwa watu bilioni 2.5 ndani ya miaka 50 ijayo.

**MKASA WA 'BONGE'**

Ukimuona kijana huyo kwa mara ya kwanza, mshangao ni jambo la lazima. Ni mnene kupita kiwango unachokifahamu! Ndivyo ulivyokuwa ushuhuda wa gazeti Nipashe.

Huyo ni Mussa Mkunda (31), mkazi wa Kata ya Mzinga, Magole wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, mwenye unene na uzito kupindukia, ni kati ya wanaoishi kwa tabu hata kushindwa kujishughulisha kwa maisha ya kawaida.

Akizungumza na mwandishi wa makala hii, akiwa amelazwa jengo la Mwaisela, wodi namba tano katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa ajili ya uchunguzi baada ya kubinika anaongezeka uzito, anajitambulisha kuwa na uzito kilo 162.3.

Kijana huyo anasema, ameishi na uzito huo kwa takribani miaka 20, jambo linalomzuia hata maisha ya kawaida ya kwenda kujitafutia riziki, kama ilivyokuwa kwa vijana wengine.

"Nilizaliwa na mwili wa kawaida, lakini kadri ninavyokuwa mwili unaongezeka, ushauri wa madaktari ambao nimeambiwa niufuate unahitaji fedha, sababu vipimo ni fedha.

"Mwili ni mkubwa hata kazi nitanya kazi ipi, nachoka sana muda mwingine, nilikuwa namtegemea mama mzazi kunihudumia, alikwishafariki, anaeleza kijana huyo.

Mkunda anarejea maelezo ya madaktari wake, uzito, umri na urefu alipo haviendani, hivyo anahitajika kufanyiwa uchunguzi kubaini undani wa tatizo lake.

"Nimeandikiwa vipimo karibia tisa, Sina utaalamu sana ila nimeambiwa niangalie kiwango cha 'cholestrol', kupima moyo, ini, figo. Gharama hawakunitajia, lakini nina imani bima itanisaidia....," anasema, katika kauli ya kulalamika. Katika hilo anaiomba jamii kumchangia fedha ajiunge na huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kupunguza makali ya gharama za matibabu yake.

Mkunda ana maoni kwamba ndio njia sahihi itakayomsaidia kupata matibabu endelevu ikiwamo kuhudhuria kliniki, kwa kadri atavyoshauriwa wa madaktari.

"Hapa nilipo siwezi kupata kazi wakikataa nikienda kuomba kazi katika usafiri wa daladala inabidi siti ya watu wawili nikae peke yangu," anasema.

Hadi juzi, Nipashe ilitaarifiwa hospitalini Muhimbili, kwamba Mkunda alipatikana na athari za choletsral mwilini na karuhusiwa kutoka wodini Mwaisela, kuendelea na tiba ya kawaida.

**MUUGUZI**

Amani Kuziganika ambaye ni Muuguzi Msaidizi wa wodi ya Mwaisela, alikolazwa Mkunda, anasema kijana huyo alipokewa Novemba 12, mwaka huu, akitokea Hospitali ya Mnazi Mmoja Dar es Salaam.

"Ameshaanza vipimo, lakini kutokana na alivyoelezea uwezo wake kiuchumi, tumemuandikia barua mkurugenzi kuhusu suala hili ili kuangalia utaratibu upi utatumika," anasema Kuziganika.

Mfuko wa bima ya afya kupitia vifurushi tofauti, hutoa huduma za matibabu kwa gharama anazomudu mwanachama, kulingana na vigezo ilivyoweka ikiwamo umri.

Anataja vifurushi hivyo na gharama zake kwa mtu mmoja vipo vya Sh. 192,000; Sh. Sh. 384,000 na Sh. 516,000, vyote vinadumu mwaka mmoja kwa kila kifurushi.

AFYA

## USHUHUDA WA MBEYA...

# Kusambazwa umeme kunavyookoa uhai katika vituo vya afya Kigoma

## • Wanufaika wakiri amani mlangoni

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

UMEME ni nishati muhimu inayopaswa kupatikana katika maeneo yote yanayotoa huduma za afya, hususani ngazi ya Kituo cha Afya na nyinginezo, kutokana na huduma za afya ya uzazi kuitegemea katika utekezaji malengo yake.

Hata hivyo, hadi sasa kuna maeneo muhimu ya mkoa, nishati haipo katika baadhi ya zahanati na vituo vya afya, jambo linalosababisha adha kubwa kwa kinamama wajawazito, pindi wanaposhindwa kujifungua kwa njia ya kawaida na kuhitaji upasuaji.



Meneja wa Shirika la World Vision Mkoa wa Kigoma, Makoye Kaniki (kushoto), alipomkabidhi Mganga Mkuu wa Wilaya Kasulu, Robert Rwebangira, mzani wa kuwapima wajawazito, katika Kituo cha Afya Kimwanya. **PICHA: WORLD VISION.**

**DC UVINZA**

Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Mwanamvua Mrindoko, anasema kukoseka nishati hiyo katika baadhi ya maeneo wilayani Uvinza, ni kikwazo dhidi ya uboreshaji huduma za afya, hasa kwa wajawazito na watoto

Katika kuhakikisha tatizo hilo linatokomezwa, Mrindoko anawaomba wadau wote wanaopanga kutekeleza miradi mbalimbali wilayani kuzingatia vipaumbele muhimu katika maandiko yao ya miradi, wakiwasiliana na serikali ya wilaya, ili wajadiliane kupata mwelekeo wa mafanikio.

Mrindoko anasema, kwa sasa wadau wanapaswa kuwekeza kusaidia uboreshaji huduma za afya na hasa upande wa kufunga nishati umeme jua katika maeneo ambayo umeme halisi hauwafikii, ili wananchi waipate huduma hiyo muhimu.

"Ni sawa serikali imefanya maboresho mengi katka sekta ya afya ikiwamo kusambaza umeme wa REA katika maeneo ya vijijini, lakini bado kuna maeneo nishati hiyo haijafika. Hivyo, bado tunahitaji jitihada za wadau wa maendeleo katika kutatua tatizo hilo," anasema Mrindoko.

Kukosekana nishati hiyo kumechangia baadhi ya wajawazito kuathirika na matatizo ya uzazi, kama vile kutokwa damu nyingi wakati wa kujifungua, njiani wakielekea vituo vya afya vyenye umeme na vinatoa huduma ya upasuaji.

**MRADI WORLD VISION**

Ni hatua iliyoifanya shirika la World Vision Tanzania kupitia mradi wake wa Sustain Kigoma, inatekeleza programu za kuboresha mifumo ya upatikanaji na matumizi ya huduma bora za afya ya uzazi mkoani.

Hiyo ni utekelezaji wa programu mbalimbali za kuboresha mifumo ya upatikanaji na matumizi ya huduma bora za afya ya uzazi kimkoa.

Anataja mradi mmojawapo ni ufungaji umeme unaotumia mionzi ya jua kwenye maeneo ya kutoa huduma za afya yasiyokuwa na umeme.

Hapo inalenga kuondoa adha kwa wananchi wa maeneo hayo, waliokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma za afya zinazotegemea umeme.

Inaelezwa, mradi umeshajenga wodi za wajawazito na majengo ya upasuaji katika vituo vya Kimwanya, Kagezi na Gwanumpu, huku kukitajwa.

Mbali na kuwapo shule za sekondari 65 na zahanati 96 mkoani Kigoma, kuna vituo vya afya vilivyonufaika na mradi ambavyo ni Kalya, Bitale, Gwanumpu, Kagezi, Nyamidaho, Mwamgongo, Buhingu, Uvinza, Kimwanya, Nyakototo, Rusesa, Muyama, pia Jandana Ilagala.

Meneja wa World Vision Mkoa wa Kigoma, Makoye Kaniki, anaahidi kushirikiana na serikali kutatua masuala ya maendeleo kwenye jamii na anawaomba viongozi wa serikali kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia miradi hiyo, ili iwanufaishe wananchi wa muda mrefu.

"Tumetekeleza miradi hii muhimu kwa afya ya mama na mtoto, tunaomba usimamizi mzuri ili kuudhibiti uharibifu," anasema.

Ni mradi unaotekelezwa kwa miaka minne sasa na unakamilika mwaka huu, kwa gharama ya Dola za Canada11,911,394, inayokadiriwa sana na fedha za Kitanzania shilingi bilioni 21

"Tumetekeleza miradi hii muhimu kwa afya ya mama na mtoto, tunaomba usimamiaji mzuri ili kudhibiti uhalibifu," anasema.

**MENEJA MRADI**

Meneja Mradi wa Sustain Kigoma, Dorothea Sago, anasema umewasaidia huduma muhimu zilizokuwa hazifanyiki katika vituo vya afya na zahanati

Anazitaja baadhi ya mafanikiwa ni mradi wa upasuaji, hifadhi ya damu salama na hifadhi ya chanjo zinazotumika kwa wajawazito na watoto, pia uhakika wa mwanga muda wa usiku.

Dorothea anataja lingine la mafanikio, kwamba ni kuwajengea uwezo watoa huduma wa zahanati, vituo vya afya na hospitali, kwa kuwaongeza ujuzi binafsi.

Analitaja hilo kwenda sambamba na ununuzi wa vifaa kama vile mashine za kupumulia, mashine za kutoa dawa za usingizi na mizani ya wajawazito na watoto.

Wasimamizi wa Kamati za Afya za Wilaya na Mkoa (RCHMT), wameongezewa ujuzi kwenye usimamizi bora na wenye matokeo chanya, katika kuwaelimisha wananchi kuanzisha vikundi vya uhamasishaji kuwa 'baba bora.'

**WANUFAIKA**

Anastazia Raymond, mkazi wa Kata ya Kalya, ambayo kabla ya utekelezaji mradi wa Sustain Kigoma, hapakuwapo nishati ya umeme, anaeleza ilikuwa shida kwa wajawazito, kutokana na ukosefu wa huduma za dharura, pindi linapotokea tatizo

Anastazia anasimulia, kutokana na eneo hilo kuwa na miundombinu duni ya barabara, iliwalazimu kutumia usafiri wa majini walipokodi boti kuzifuata huduma zilipo, iliyochanga hata ajali zenue maafa, njiani.

Mkazi huyo, anakiri walikutana na magumuya usafirishaji, pia gharama kubwa kutoka eneo umbalo zaidi ya kilomita 270, kwenda kuzipata huduma wilayani Kigoma na wengi walishindwa kumudu.

''Tulikuwa tunatumia gharama kubwa sana wakati mwingine zaidi ya laki moja kumsafirisha mwanamke mjamzito, ili kuokoa maisha yake," anaeleza.

Mkazi mwingine wa kata hiyo, Zabibu Jafari, anaeleza shaka ya wananchi wa eneo hilo umeisha tangu umeme wa mionzi ya jua ufungwe katika kituo cha afya Kalya, kwani huduma muhimu zinapatikana haraka.

''Hatuna tena wasiwasi katika masuala ya uzazi tofauti na awali, hivyo tunashukuru kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na wadau wa afya na serikali, "anasema, akikumbuka zama zilizopita, zilitumka hata mwanga wa tochi.

Ni taarifa ya Dk Nasoro Matuzya, aliyekuwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, wakati wa makabidhiano ya mradi katika Kituo cha Afya cha Kalya kabla hajahamishiwa eneo lingine.

AliaInisha adha, kwamba umbali kutoka Kalya hadi Kigoma ni zaidi ya kilomita 270 na barabara zilikua mbovu na hazipitiki kirahisi, hivyo uliowekwa umeme umeongeza ufanisi wa huduma.

''Mwaka huu tumepata vifo viwili tu, wakati mwaka juzi tulikuwa na vifo 11. Utaona jinsi gani uwapo wa umeme umepunguza vifo kwa wanawake wajawazito, kwani wengine walikuwa wanapoteza maisha wakiwa njiani kwenda kufuata huduma za upasuaji," anasema

Pia, kunaelezwa idadi ya wanawake wanaojifungua katika kituo hicho cha afya, imeongezekakutoka vizazi 25 hadi kati ya 40 na 50 kwa mwezi, kwani wanawake wana uhakika wa huduma za dharura, mahalo walipo.

Kukosekana kwa nishati umeme katika vituo vya afya na zahanati, kunatajwa kuwa kikwazo kikubwa dhidi ya afya ya mama na mtoto, hivyo hatua mbalimbali zinapaswa kuchukuliwa.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alipomjulia hali mtoto Athumani, aliyekuwa na umri wa wiki mbili katika Kituo cha Afya Uvinza na aliyembeba, ni mama yake, Esil Amour. Makamu wa Rais alitembelea kulipokuwapo mradi wa upanuzi. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS.**

MAZINGIRA

# Uswisi wajiunga mradi shirikishi unaosimamia ustawi msitu vijijini

## • Kilolo wachekelea mwanzo wa kwao

**Na Christina Mwakangale**

JE, unaijua Miradi ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii Tanzania au maarufu USMJ, ambayo inatekelezwa nchini?

Hii imekuwa ikisaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na sasa kunashuhudiwa ikitekelezwa kwingi.

Ni orodha inayojumuisha, Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania (TTCS) na ule wa Kuhifadhi Misitu kwa Kuwezesha Biashara Endelevu ya Misitu (CoFoREST).

Kimsingi, ni miradi inayotekelezwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na Shirika la Kuendeleza Nishati Tanzania (TaTEDO) na yote iko chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC) na kuratibiwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu Asili Tanzania (TFCG).



Ndivyo yalivyo mazingira ya misitu wilayani Kilolo, Iringa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Ni kauli inayotolewa na Peter Sidler, Mkuu wa Idara ya Ajira na Kipato kutoka Ubalozi wa Uswisi nchini, kwa kamati ya ushauri ya mradi iliyotembelea kijiji cha Mahenge, kilichopo katika Kata ya Mahenge, wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Anasema, binafsi anaridhishwa na miradi wanayoifadhili na inawapa hamasa kuendelea nayo, akisema ushirikiano wa nchini na Uswisi, hadi sasa una zaidi ya miaka 30, wakiwa na matarajio ya kuendelea hasa katika kugusa kundi kubwa la jamii lililopo vijijini.

Mwakilishi huyo anasema, takwimu zinaonyesha Tanzania ni imo katika nchi zinazoongoza kwa uharibifu wa misitu na anafafanua:

"Shughuli za uhifadhi zinazofanyika Kijiji cha Mahenge zimeonyesha kuwa, jamii ipo tayari kutunza na kuhifadhi misitu yao na kunufaika, hivyo tutaendelea kuziwezesha taasisi kama TFCG na MJUMITA, kuendeleza malengo ya wanavijiji."

Rai yake ni kwamba, Idara ya Misitu ikishiriksha jamii, itachochea mabadiliko kuhifadhi, kiuchumi na kijamii.

"Sisi kama Ubalozi wa Uswisi, tunaridhishwa na hali ya USMJ inayotekelezwa kwa vijiji vya mradi jambo ambalo linatupa nguvu kuendelea kufadhili kwani ni njia muhimu ya kupunguza umaskini na kuongeza uhifadhi," anasema.

Pia, anautaja ubalozi unasaidia uhifadhi na kuboresha maisha ya wananchi, akiwa na ufafanuzi: "Ni vyema wadau wote wakashiriki katika uhifadhi, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo yana madhara makubwa duniani kwa sasa."

"Tanzania imejaliwa misitu mingi ambayo ikitunzwa vizuri, itaweza kuchochea uwepo wa hali ya hewa nzuri," anaendelea.

MHIFADHI MISITU

Mkurugenzi wa TFCG, Charles Meshack, anasema Tanzania ina hekta milioni 48.8 za misitu, kati yake hekta milioni 22 ni ardhi za vijiji na hekta milioni tano zimo kwenye eneo la mradi shirikishi USMJ, huku hekta milioni 17 hazipo kwenye usimamizi.

Anabainisha kwamba, TFCG na MJUMITA wameamua kuja na miradi ya TTCS NA CoFoREST, ili kuwawezesha wananchi kutambua umuhimu wa utunzaji misitu.

Meshack anasema, iwapo hakutakuwapo jitihada za kuhifadhi misitu ndani ya miaka 40 ijayo, misitu hiyo itakuwa imetoweka kwa kuwa hivi sasa kila mwaka, kuna hekta 469,000 zinazopotea.

"Miradi hii ambayo tunawapelekea wananchi ina malengo makuu matatu, ambayo ni kuwahamasisha wananchi kuhifadhi misitu ya asili; kuvuna kwa uendelevu na wanapovuna kwa uendelevu kipato wawekeze kwa shughuli za wananchi na uhifadhi.

"Pia, kuna kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili nchi isiwe jangwa. Lengo kubwa ni kuwapa wanavijiji motisha wasigeuze misitu mashamba badala yake waweze kuvuna kwa uendelevu mkaa na mbao," anasema Meshack.

Mkurugenzi huyo anasema, miradi ya USMJ kwa miaka saba sasa, imechochea maendeleo, kukuza uchumi na kasi ya uhifadhi na anavitaja vijiji zaidi ya 30 vinavyotekeleza mradi huo, sasa vimeboresha sekta za elimu, afya, maji, kilimo na mikopo, wanavijiji wakiwa wamekusanya zaidi Sh. bilioni tatu.

"Tumewekeza takribani bilioni 12 kwa awamu ya kwanza na pili, pia zaidi ya Sh. bilioni tatu zimepatikana," anasema Meshack.

Pia kwa awamu ya tatu wanatarajia kuwekeza sh. bilioni saba kwa kipindi cha miaka mitatu na kujikita kujengea uwezo wataalamu, ili kutekeleza.

Mkurugenzi huyo anasema, kupitia miradi hiyo wamefanikiwa kurasimisha ardhi za vijiji kuwa za kisheria, jambo linalotaka uhakika wa kupangia kazi kisheria.

Anashauri serikali itoe kipaumbele katika sekta ya mazingira na misitu, ili ziwe endelevu na kuondoa sheria vikwazo katika usimamizi wa misitu.

Mkurugenzi wa MJUMITA, Rahima Njaidi, anasema asasi hizo zimedhamiria kuleta mabadiliko kwenye sekta ya misitu na mazingira nchini.

**RAS IRINGA**

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Elia Luvanda, anaipongeza Uswisi, TFCG, MJUMITA na wadau wengine kutekeleza mradi huo, kwani unabeba umuhimu wa maendeleo.

Anaahidi mkoa kushirikiana na wadau wote wanaodhamiria kuhifadhi na kutunza misitu.

Ofisa Maliasili wa Mkoa wa Morogoro, Joseph Chuwa anawataka wanakijiji wa Mahenge kutumia fursa ya mradi huo kufanya mabadiliko chanya kijijini hapo.

"Mimi nipo Morogoro, natambua faida za hii miradi nawaomba msirudi nyuma kwani ina faida ya kiuchumi, kijamii maendeleo na uhifadhi," anasema Chuwa.

Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Utafiti Tanzania (TAFORI), Dk. Charlestino Balama anawashauri wataalamu na wananchi kutafuta watafiti, ili kuweza kubaini fursa zote zilizopo katika misitu wa Mahenge.

"Watafiti tunapaswa kuja huku kwenye msitu wa Mahenge kwani kuna fursa nyingi nimeziona hapa kama kuwapo vipepeo, ufugaji nyuki, madini na vingine vingi," anasema Dk. Balama.

**WILAYANI KILOLO**

Mtaribu wa Mradi wa CoFoREST wilayani Kilolo, Mkoa wa Iringa, Aigen Mwilafi, anasema mradi huo umewezesha kuandaa mipango ya USMJ na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Anasema, hadi sasa kuna jumla ya misitu 11 ambayo haijatengwa kuwa ya hifadhi ya vijiji na mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu ya vijiji 45 ikipitwa na wakati na inahitaji kuhuishwa.

"Tunaomba muendelee kushirkiana nasi katika kutekeleza hayo," anasisitiza Dk. Balama na anaongeza:"TFCG na wadau wake kupitia mradi huu, mpaka sasa imeweza kuwajengea uwezo watalaamu 17 kutoka ngazi ya halmashauri na wanne kutoka ngazi ya kata kwa kutoa mafunzo mbalimbali.

"Kijiji cha Mahenge ambacho ndicho kinatekeleza mradi huu kumefanyika mikutano ya vitongoji kwa ajili ya kuutambulisha mradi.

"Pia, kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu ya kijiji na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mahenge, wilayani Kilolo, Said Mhina, anaomba ridhaa ya kutolewa mafunzo, akiamini yatasaidia kuleta maendeleo ya kijiji hicho.







# Wizara Afya yataja maeneo 9 ya kipaumbele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetaja maeneo tisa ambayo yataendelea kupewa kipaumbele katika sekta ya afya kwa miaka mitano ijayo ikiwamo kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Mabula Mchembe, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa 21 wa kitaalamu wa tathmini ya utekelezaji katika Sekta ya Afya ulioandaliwa kwa pamoja na wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na wadau mbalimbali.

Alisema kikao hicho kinalenga kuweka mikakati ya nini kifanyike miaka mitano ijayo, baada ya kupitia mikakati ya miaka mitano iliyopita na kuona mafanikio na vikwazo vyake.

Alitaja maeneo ambayo wizara itayaangalia kwa miaka mitano ijayo katika uboreshaji wa huduma zinazotolewa ikiwamo huduma za chanjo, utoaji wa huduma hospitali unaofanywa na watumishi wa afya.

"Pia dawa, vifaa na vifaa tiba katika uboreshaji wa utoaji huduma," alisema.

Prof. Mchembe alisema mpango mkakati wa tano unaoenda kuanza ni matokeo ya nne, unaangazia mafanikio na kuboresha maeneo yaliyokuwa na vikwazo na kuweka mikakati madhubuti ya kuboresha Sekta ya Afya.

"Kikao hiki cha siku tatu kitakuwa kinaangalia tunafanya nini katika kuboresha huduma ya mama na mtoto, huduma kwenye hospitali zetu na matibabu ya kibingwa, kikubwa ni uboreshaji wa huduma kwa wananchi wetu," alisema.

Naye, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya afya kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dk. Dorothy Gwajima, alisema wakiwa wasimamizi wa utekelezaji wa sera katika ngazi za mikoa na mamlaka za mitaa wapo tayari kutekeleza maagizo na miongozo itayotolewa kupitia kikao hicho.

"Katibu Mkuu Wizara ya Afya ameeleza mambo mengi, sisi tupo kama wadau ambao tunasimamia utekelezaji kwenye ngazi ya mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa tunasubiri maelekezo na miongozo ya kisera, ili kwenye kipindi cha miaka mitano ijayo tuweze kutekeleza kwa kasi ile ile," alisema.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Afya, Edward Mbanga, alisema kikao hicho hupokea mambo yote katika sekta ya afya yaliyofanyiwa tathmini na yaliyokubalika kuwa ndio yatakuwa malengo na mwelekeo wa sekta hiyo nchini.



Baadhi ya wachuuzi wakinunua mananasi katika soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana, moja linauzwa kwa Sh. 500 hadi Sh. 1,000 kabla ya msimu lilikuwa Sh. 1,500 hadi Sh. 2,000. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwongozo udhibiti rushwa wazinduliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa kudhibiti rushwa kwenye manunuzi yanayofanywa na taasisi za umma kutokana na asilimia 10 ya tuhuma za rushwa kuhusisha ununuzi wa umma.

Akizindua mwongozo huo jana, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Tixon Nzunda, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), kuchukua hatua ili kudhibiti rushwa kwenye ununuzi.

Alisema serikali inatambua kuwa rushwa ni tatizo kubwa linaloathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii na imekuwa ikifanya jitihada za mara kwa mara za kuhakikisha kero hiyo inadhibitiwa.

Alizitaka idara za ununuzi kuhakikisha asilimia kumi ya malalamiko yanayohusu vitendo vya rushwa iliyotolewa na TAKUKURU inashuka kwa kutumia mwongozo huo.

Alisema endapo taasisi hizo zitazingatia mwongozo huo, vitendo vya rushwa vitapungua na serikali itatimiza malengo yake ya kimaendeleo.

"Naomba wadau wote mtumie mwongozo huu kama zana ya kimenejimenti na kiutawala kudhibiti kuzuia na kuchukua hatua za kiutawala kupambana na rushwa kwenye ununuzi," alisema Nzunda.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Mhandisi Ayoub Kasuwi, alisema licha ya kuwapo kwa kero katika ununuzi wa umma, ushirikiano wa PPRA na TAKUKURU umechangia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mianya ya rushwa.

Mhandisi Kasuwi alisema kiwango cha ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kimeongezeka kutoka asilimia 39 kwa mwaka wa fedha 2006/7 na kufikia asilimia 78.8 mwaka wa fedha 2019/20.

Alisema mwongozo huo utakuwa na mchango mkubwa wa kuongeza ukidhi wa sheria ya ununuzi wa umma na kuziba mianya ya rushwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema mkakati wa kupambana na rushwa unamtaka kila mdau katika eneo lake kuhakikisha amejiwekea mpango kazi wa kudhibiti vitendo hivyo.

Alisema kwa kuzingatia wajibu wa kisheria, TAKUKURU, kupitia mshauri elekezi SPA Infosuv East African Limited, chini ya usimamizi wa PPRA ilifanya utafiti ulioshirikisha wadau 368 kutoka makundi yote muhimu katika ununuzi wa umma kwenye mikoa 23 yaTanzania Bara na kuandaa mwongozo huo.

## Ashauri wabunifu kutumika kupata ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Goodiel Moshi, ameiomba serikali kuwatumia wabunifu mbalimbali nchini ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Dk. Moshi aliyasema hayo juzi jijini Dodoma, wakati alipokuwa akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano na maonyesho ya vijana wabunifu na wajasiriamali ulioandaliwa na Kituo cha Capital Space.

Alisema serikali inatakiwa kuwawezesha vijana wabunifu, ili wawe na uwezo wa kuzalisha bidhaa zitakazokidhi mahitaji katika jamii zao.

Alisema kama wabunifu nchini watashindwa kuzalisha bidhaa zenye mahitaji katika jamii zao watashindwa kufanikiwa kutokana na kukosa soko.

"Vijana wetu wabunifu pamoja na wajasiriamali mnatakiwa kubuni bidhaa zinazolenga mahitaji katika jamii zetu, lazima muone ni jinsi gani ya kuwafikia kina mamalishe, wakulima pamoja na makundi mengine," alisema.

Alisema kama wabunifu nchini watashindwa kulenga mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii zao bidhaa zao hazitadumu kutoka na kukosa watumiaji.

"Ni tatizo kwetu sote kuona ni jinsi gani tunasaidia wabunifu wetu kutengeneza bidhaa zitakazohitajika na jamii," alieleza Dk. Moshi.

Mtendaji Mkuu na Mwanzilishi wa Kituo cha Capital Space, Abdallah Mbwana, alisema lengo ni kuwawezesha vijana kutatua matatizo katika jamii kwa kutumia ubunifu wao.

Alisema, mpaka sasa wameanzisha programu mbalimbali za kuwafikia vijana wabunifu pamoja na wajasiriamali kutumia ujuzi walionao ili kutatua matatizo yaliyopo katika maeneo yao.

"Tangu Capital Space kuanzishwa tumekuwa tukisaidia vijana wabunifu na wajasiriamali kutoka katika maeneo mbalimbali kwa kuwajengea uwezo na kuwawezesha kuongeza maarifa katika kazi zao," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa Mfuko wa Ubunifu wa Maendeleo ya Binadamu (HDIF), Joseph Manirakiza, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili namna ya kutumia teknolojia kubuni bidhaa zitatatua matatizo ya jamii.

Alisema matatizo hayo ni pamoja na yaliyopo katika sekta ya elimu na huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi.

"Sisi kama shirika tayari tumekuwa tukiwezesha jamii katika maeneo mbalimbali kama vile elimu na huduma za maji, ambapo tumewezesha kubuniwa kwa mfumo wa teknolojia ya malipo katika huduma za maji pamoja na mfumo wa kufuatilia wajawazito," alisema.





## Dk. Tulia aanza kuboresha sekta afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, amesema anaanza rasmi kuwahudumia wananchi wa jiji hilo, akianzia kuboresha sekta ya afya kwa kuandaa mfumo maalumu wa kuwasaidia wananchi wote kuwa na bima ya afya.

Dk. Tulia ambaye ni Naibu Spika alisema ataanza kutekeleza azma yake hiyo kwa watu 1,000 ambao atawaunganisha na huduma hiyo ya bima ya afya na kuendelea na makundi mengine ya wananchi.

Alisema ataanza kwa kuwalipia huduma hiyo katika awamu ya kwanza na kisha utaandaliwa utaratibu maalumu ambao wananchi watakuwa wanajilipia Sh. 100 kila siku itakayowawezesha kujilipia katika miaka mingine bila kulipa fedha zote kwa mkupuo.

Alisema Jiji la Mbeya lina vituo vingi vya kutolea huduma za afya zikiwamo zahanati, vituo vya afya na hospitali, lakini baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu huduma za matibabu kwa sababu ya kutokuwa na bima.

"Nimekuwa nikipita kwenye vituo mbalimbali na kukutana na matatizo ya wananchi kulalamika kushindwa kulipia baadhi ya huduma kwa sababu ya gharama kubwa, sasa tumeona njia nzuri ya kuwaondoa kwenye tatizo hilo ni kuhamasisha bima ya afya," alisema Dk. Tulia.

Alisema vipaumbele vingine atakavyoanza navyo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya barabara ili kuondoa msongamano wa magari katikati ya jiji hilo na kuwarahisishia wananchi usafiri.

Vilevile, alisema atahakikisha anashirikiana na wadau mbalimbali pamoja na serikali kuboresha sekta ya elimu katika jiji hilo, kwa kuhakikisha walimu wanakuwa na ofisi nzuri ili wapate hamasa ya kufanya kazi.

Katika hatua nyingine, Dk. Tulia alisema ili kuhakikisha anazipata kero za wananchi, ameanzisha utaratibu maalumu wa kusikiliza kero za wananchi wa jimbo hilo kila siku ya Alhamisi na Jumamosi kwenye maeneo mawili tofauti.

Alisema maeneo yatakayotumika ni Ofisi ya Mbunge ambayo itakuwa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya na itatumika Alhamisi na Jumamosi itatumika Ofisi ya Taasisi ya Tulia Trust iliyopo katika Kata ya Uyole.

Alisema kipindi ambacho atakuwapo jimboni atakuwa anasikiliza kero hizo yeye mwenyewe na siku anapokuwa bungeni ama kwenye shughuli zingine za kitaifa kero hizo zitasikilizwa na wasaidizi wake.

# TFRA yaridhishwa usambazaji mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea nchini (TFRA), imesema imeridhishwa na kasi ya usambazaji wa mbolea katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa kilimo.

Mamlaka hiyo pia imewataka wafanyabiashara wa mikoa hiyo kusambaza mbolea hizo mpaka maeneo ya vijijini, ili kuwarahisishia wananchi kupata kwa gharama nafuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephano Ngairo, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipofanya ukaguzi wa upatikanaji wa mbolea kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa hiyo na kusema kwa sasa mahitaji ya wakulima ni makubwa.

Alisema katika maghala mbalimbali walikopita kukagua, walibaini uwapo wa mbolea ya kutosha, huku wakulima wakiendelea kununua mbolea ya kupandia mazao.

"Pamoja na kwamba kwa sasa ni msimu wa kupanda, lakini kwenye maghala tumekuta zipo mbolea nyingi zikiwamo hata za kukuzia, sasa ninachowaomba wafanyabiashara ni kuendelea kuleta mbolea hizo, ili wakulima wanapozihitaji wazipate kwa urahisi," alisema Dk. Ngairo.

Aliwataka wakulima kuzingatia kanuni za kilimo bora ili kuongeza tija ikiwamo kufanya uchaguzi sahihi wa mbegu, kupalilia kwa wakati pamoja na kupandia mbolea na kukuzia kwa wakati mazao yao.

Baadhi ya wamiliki wa maghala ya kuhifadhia mbolea mkoani Mbeya, walisema pamoja na kupokea mbolea za aina tofauti kwa wingi pia kasi ya wakulima kununua bidhaa hiyo ni kubwa na inaridhisha.

Mmoja wa wakulima hao, Edwin Zenge, alisema mpaka sasa wamepokea zaidi ya tani 1,000 za mbolea tofauti zikiwamo za kupandia aina ya DAP na za kukuzia aina ya Urea pamoja na mbolea zenye virutubishi tofauti.

Alisema kasi ya wananchi kununua bidhaa hiyo ni kubwa na inawahamasisha wafanyabiashara hao kuongeza kasi ya uagizaji ili kuwahudumia vizuri wananchi wa mkoa huo.

"Hili ghala lilikuwa limejaa mpaka juu, lakini ndani ya muda mfupi tumebakiwa na shehena hii ndogo kutokana na wakulima wengi kuchangamka kuja kuinunua, hii kwetu ni changamoto kubwa sana," alisema Nzege.

Hivi karibuni baadhi ya wakulima waliiomba serikali kuwasaidia kusambaziwa mbolea mapema na kuwadhibiti wafanyabiashara wasipandishe bei kiholela wakihofia kushindwa kufikiwa kirahisi na bidhaa hiyo baada ya mvua.

Hata hivyo, Dk. Ngairo alisema wafanyabiashara wanatakiwa kuuza bidhaa hiyo kwa kuzingatia bei elekezi huku akisisitiza kuwa bei elekezi inaruhusiwa kufanyiwa marekebisho na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa na wilaya pekee.



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, akiwaangalia watoto wanne mapacha wa Stella Kalinda (32), alipowatembelea katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya jana, ambako wamelazwa na mama yao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wabunge wamsaidia aliyejifungua watoto 4

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WABUNGE wawili mkoani Mbeya wamemtembelea Stella Kalinda (32), mkazi wa Kijiji cha Idendeluka katika Kata ya Sangambi, wilayani Chunya ambaye alijifungua watoto wanne kwa mpigo hivi karibuni na kumpatia msaada kwa ajili ya malezi ya watoto hao.

Wabunge hao ni wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka na wa viti maalumu, Maryprisca Mahundi, walimtembelea mama huyo juzi katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya, alikolazwa na watoto hao kwa uangalizi.

Wakizungumza baada ya kumpatia msaada mama huyo, wabunge hao waliwaomba Watanzania kuendelea kumsaidia mwanamke huyo kutokana na gharama za malezi ya watoto kuwa kubwa.

Mahundi alisema kwa kawaida mwanamke akiwa mjamzito anategemea kupata mtoto mmoja ama wawili, lakini kwa mwanamke sio la kawaida na kutakiwa kusaidiwa.

Alisema kupata watoto wanne kwa mwanamke ni furaha kubwa, lakini kiafya inaweza kuwa hatari endapo hatapata huduma bora za afya, aliwapongeza madaktari wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa huduma waliyompatia.

"Mimi kama mwanamke mwenzake nimeguswa sana na mwenzangu huyu kwa zawadi aliyoipata, sisi tumekuja kumwona, lakini tutamsaidia hata makopo kadhaa ya maziwa kwa ajili ya watoto hawa, lakini niwaombe Watanzania wengine waguswe," alisema Mahundi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Lupa, Kasaka alisema atatembelea nyumbani kwa mwanamke huyo ili aone mazingira yalivyo ili atoa msaada unaostahili.

Alisema amekuwa akifuatilia taarifa za afya ya mama huyo pamoja na watoto wake na akawaomba Watanzania wamsaidie kupata bima ya afya kwa ajili yake na watoto wake.

Stella alijifungua watoto hao wiki tatu zilizopita katika Kituo cha Afya cha Chalangwa na kuhamishiwa Hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa ajili ya uangalizi maalumu.



# ZEC yaagizwa kufuatilia hatimiliki ya maeneo yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Mohammed Salum, ameushauri uongozi wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kuyatafutia hatimiliki maeneo yote yanayomilikiwa na ofisi hiyo.

Aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika ofisi za ZEC Maisara Mjini Zanzibar ukiwa ni utekelezaji miongoni mwa maagizo ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa mawaziri wake baada ya kuwaapisha.

Katika ziara hiyo, Dk. Khalid alipata nafasi ya kuzungumza na watendaji wa tume ofisi za Unguja pamoja na kuzungumza na watendaji wa tume waliopo Pemba kwa njia ya mtandao.

Dk. Khalid aliwataka watendaji kuwa maagizo ya Rais, ni kwa ajili ya watendaji wote na kuwasisitiza kutekeleza majukumu yao kwa kutumia mpango kazi unaokwenda sambamba na ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020/2025.

Aidha, Dk. Khalid aliwataka watendaji kutumia ubunifu katika kutekeleza majukumu yake na kuipongeza Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa ubunifu wake wa kurahisisha mawasiliano kwa kupunguza gharama za kusafiri wafanyakazi kwa vikao vya kawaida na badala yake kufanya vikao, hivyo kwa kutumia mtandao.

Aliitaka tume hiyo kukutana na wadau kwa ajili ya kukusanya maoni yao juu ya utekelezaji wa majukumu yake sambamba na kuwasisitiza suala la kutoa habari kwa wananchi.

Hata hivyo, Dk. khalid aliwataka waandishi wa habari kuacha kupotosha umma kwa kuandika taarifa za uongo pamoja na kuwatahadharisha wananchi katika kusambaza taarifa na kutumia vibaya mitandao ya kijamii, jambo ambalo linaweza kuharibu amani ya nchi.

Waziri huyo aliwataka watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kujenga umoja na kushirikiana, ambapo aliahidi kumchukulia hatua mfanyakazi yeyote atakayevuruga na kutoa siri za taasisi yake.

Aidha, alieleza kufurahishwa na utendaji wa uongozi wa ZEC chini ya mkurugenzi wake, Thabit Idarous Faina, kwa ubunifu na matumizi mazuri ya fedha za serikali kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha kuendesha uchaguzi na kujenga ofisi ya uchaguzi.

Naye Faina alisema tume imepata mafanikio makubwa kwa kuendesha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 bila ya vikwazo vya kiuchaguzi na kuiweka nchi katika hali ya amani na utulivu.

Faina alisema tume imeokoa jumla ya Sh. 2,464,547,631 kati Sh. 9,046,621,534 zilizokadiriwa kutumika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Faina alieleza kuwa Tume ilitumia Sh. 6,582,547,631 kwa ajili ya kuendesha uchaguzi huo pamoja na kujenga ofisi ya uchaguzi ya Wilaya ya Magharibi "A", kujenga uzio wa ofisi ya uchaguzi ya Wilaya ya Kati na kufanya ukarabati wa ofisi ya ZEC ya Pemba, ofisi ya uchaguzi Chakechake na ghala la vifaa vya uchaguzi la Micheweni.

Mkurugenzi huyo, alisema kikwazo kikubwa kikubwa kwa Tume ni ukosefu wa jengo kubwa linaloweza kukidhi mahitaji yote katika eneo moja kiasi kwamba Tume inapofika wakati wa uchaguzi hulazimika kukodi eneo jingine nje ya ofisi kuu kwa ajili ya kutoa huduma za uchaguzi kwa ufanisi.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akikabidhiwa vitendea kazi na aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Riziki Pembe Juma ambaye sasa ni Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, katika hafla iliyofanyika Mazizini Mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri afanya ziara ya kushtukiza chuo kikuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amefanya ziara ya kushtukiza katika Chuo cha Kiislamu kilichopo Kiuyu Pemba na kuangalia maendeleo ya uwezekaji wa mapaa ya majengo yake.

Akizungumza jana katika ziara hiyo, Simai alisema ni hatua nzuri iliyofikiwa kutokana na hali ilivyokuwapo awali kwani paa zilikuwa zinavuja, na kuagiza sehemu zilizobaki kuendelea kuzimalizia ili kuwasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu zaidi.

Waziri huyo alieleza kutoridhishwa na hali ya usafi katika maeneo ya mabweni ya chuo hicho, na kuutaka uongozi kulisimamia kwa karibu ili kuepusha uwezekano wa magonjwa ya mlipuko yanayoweza kutokea. Pia aliwataka walimu na wafanyakazi wote wa wizara hiyo, kukubaliana na wakati uliopo, na kuwataka kubadilika kwa kufuata sheria na kanuni ziliopo ili kuleta maendeleo katika sekta ya elimu.

Katika hatua nyingine, Waziri Simai akiwa na Ofisa Mdhamini Wizara hiyo Pemba, Mohammed Nassor, alitoa maelezo juu ya ujenzi wa uzio wa chuo hicho ambao ulikuwa umesitishwa kutokana na mgogoro na wananchi ambao kwa sasa upo katika hatua za mwisho kutatuliwa ili ujenzi wa uzio huo uendelee kwa lengo la kuzuia uvamizi wa eneo la chuo.

Wakati huo huo, Waziri Simai aliwakagua walimu wa madarasa ya msingi wanaoendelea na mitihani katika ukumbi wa chuo hicho pamoja na Shule ya Maandalizi Kiuyu. Naye Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Kiuyu, Mkasha Sharif Hamad, alipongeza ziara ya waziri, na aliahidi kuyafanyia kazi yale yote aliyoyaagiza ili kwenda sambamba na maagizo ya Rais wa Zanzibar.

Waziri Simai alifanya ziara pia katika Shule ya Sekondari Madungu na kuwapa ushauri wanafunzi wa kidato cha nne wanaoendelea na mitihani, kwa kuwataka kufuata sheria zote za mitihani ili kufaulu vizuri.

## Waziri asikitika ubovu wa meli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Rahma Kasiim Ali, amesikitishwa na ubovu wa mashine ya meli ya MV Mapinduzi namba mbili, ambayo ilinunuliwa na Serikali ya Zanzibar mwaka 2015.

Waziri alieleza masikitiko yake juzi alipofanya ziara ya kuzitembelea taasisi zilizomo chini ya wizara yake likiwamo Shirika la Meli na Bandari ya Malindi Zanzibar.

Alisema anasikitishwa na meli hiyo kushindwa kuendelea kwa shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa miezi miwili sasa, na kila siku meli hiyo inagharimu Sh. milioni nne kwa siku kwa ajili ya mafuta.

Naye Mhandisi Mkuu wa meli hiyo, Ramadhan Mwinyi Ramadhan, alisema jambo linalopelekea meli hiyo kuharibika mara kwa mara ilinunuliwa na kukabidhiwa ikiwa na mashine mbovu.

"Hii meli tokea ilivyonunuliwa mwaka 2015 mashine zake ni mbovu na ndio maana haifanyi safari zake vizuri," alisema mhandisi huyo.

Aidha, Waziri Rahma aliutaka uongozi wa Shirika la Meli kwenda wizarani kwa lengo la kukaa pamoja na kulijadili tatizo hilo ili meli hiyo ifanye safari zake za Unguja na Pemba.

Pia waziri huyo alifurahishwa na kasi ya uondoshwaji wa makontena katika Bandari Kuu ya Zanzibar na kumtaka Mkurugenzi wa Bandari hiyo, Nahat Mohammed Mahfoudh, kuendelea na kasi hiyo ili kuongeza mapato ya taifa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Bandari, Nahat Mohammed Mahfoudh, alisema ili kuendana na kasi ya maendeleo iliyopo, ipo haja kwa Mamlaka ya Bandari kutumia mfumo mpya wa teknolojia wa utoaji mizigo badala ya mfumo wa zamani ili kurahisisha huduma kwa watumiaji wa bandari hiyo.

Wakati huo huo, waziri huyo aliuagiza Wakala wa Barabara kuhakikisha wanaunda kamati itakayoshughulikia ukarabati wa barabara zote zenye mashimo kwa kuanza na barabara ya uwanja wa ndege ambayo imekuwa ikileta taswira mbaya ya Mji wa Zanzibar.

Kadhalika, alisisitiza wafanyakazi wa Wakala wa Barabara kupatiwa stahiki zao wanazostahili ili wafanye kazi kwa ufanisi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**



***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHAMEDI M. MJENGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0843/0041** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia SOTELE SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MBA/RB/818482/2020.**

## TANGAZO LA KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Salim Abdallah Mhene.**
Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja Namba **45 Kitalu "K" Mjini Kati Manispaa ya Shinyanga.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Salim Abdallah Mhene kwa simu namba **0763200482.**
RB Namba: **SHY/RB/2020,** Control Namba **9910819756223**

MUSA J. MAKUNDU
AFISA ARDHI
SHINYANGA.
AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

116013602

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 489 L 2020**

**ADELA FREDRICK NJAU MWOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOHN KIMARO MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**JOHN KIMARO**

**popote ulipo/mlipo**

**ADELA FREDRICK NJAU** amefungua/wamefungua shauri mbele ya baraza la Ardhi na nyumba lililopo kinondoni(mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 4.12.2021 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh Rugarabamu. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa baraza hili leo tarehe 24 mwezi 11 mwaka 2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

116013702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**

**MAHAKAMA YA MWANZO KATORO**
**WILAYA YA BUKOBA**

**MADAI:NAMBARI 13/2013**

**MDAI:TWAHA OMARY MUSHULE**

**WADAIWA:**

1: **ABDUL AHMADA MUGUNDA WA KATORO-BUKOBA**
2: **RUKUMANI OMARY WA KATORO-BUKOBA**
3: **SUDI AMRI FRESHI WA KATORO-BUKOBA**
4: **MUSSA KASIMU WA KAYANGA-KARAGWE**

Kwakua mdai ameleta madai yake ya kupinga wosia wa marehemu **OMARY MUSTAFA MUSHULE** unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama ya mwanzo KATORO siku ya tarehe 04/12/2020(IJUMAA) saa 2:00 asubuhi kujibu madai dhidi yenu.
Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 20/11/2020.

Hakimu Mahakama ya Mwanzo
KATORO
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KATORO

116013902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ABDALA ZUBERI MSANGI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 981 AMD JEIFONGO**. Chassis namba **7026.** Engine namba **6D17787400.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **KRT/RB/3350/2020.**

116013802

## KUPOTEA KWA VYETI



**ENECY MASHAKA TUYATE** anatangaza kupotelewa kwa vyeti ,cha kidato cha nne chenye index namba **SO239/0026/2015** kilichotolewa na shule ya secondary ST.FRANCIS GIRLS mwaka 2015 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0867/0661/2018** kilichotolewa na shule ya secondary PANDAHILL mwaka 2018,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **9910819755590**

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Hussein Pole**
Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba **529 Kitalu "W" Ndembezi -Mazinge Manispaa ya Shinyanga.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Hussein Pole kwa simu namba **0754923799.**
**RB** namba: **RB/SHY/2020,** Control namba **9910819752105.**

MUSA J. MAKUNDU
AFISA ARDHI
SHINYANGA.
AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

116013502


***Uza,***

***Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Uganda kukarabati reli kongwe, SGR kimya

**KAMPALA, Uganda**

BARAZA la Mawaziri nchini Uganda limeidhinisha mpango wa serikali wa kukarabati reli ya zamani kutoka Malaba mpaka wa Kenya na Uganda hadi Kampala.

Hatua hiyo inazima mpango wa awali wa ujenzi wa reli ya mwendo wa wastani -SGR, na hakuna ripoti yoyote kuhusu ujenzi wake.

Taarifa iliyotolewa mwanzoni mwa wiki na kituo cha habari cha serikali, inasema kwamba ukarabati wa reli hiyo itakuwa hatua muhimu sana katika kuimarisha shughuli ya kubeba mizigo na abiria nchini Uganda.

Taarifa hiyo inaendelea kusema kwamba reli hiyo itapunguza gharama ya kufanya biashara, kuimarisha mapato ya nchi na kuboresha maisha ya raia wa Uganda.

Ukarabati wa reli hiyo utagharimu Sh. trilioni 1.4 za Uganda na unakuja wakati Uganda inakabiliwa na gharama ghali ya kusafirisha mizigo kwa kutumia barabara.

Kwa sasa, inagharimu Dola za Marekani 3,600 kusafirisha kasha la futi 40 kutoka Bandari ya Mombasa Kenya hadi Kampala kwa kutumia barabara. Mzigo kama huo unagharimu dola 1,800.

Kulingana na muungano wa wafanyabiashara jijini Kampala - KACITA, asilimia 50 ya bei ya mizigo inayosafirishwa kutoka Mombasa hadi Kampala, ndiyo gharama inayotumika kwa usafiri.

Hivi karibuni, Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alizindua ujenzi wa reli kutoka mji wa Tororo, mpakani mwa Kenya na Uganda hadi Gulu, Kaskazini mwa Uganda.

Rais Museveni alisema kwamba usafiri wa reli ambao mara ya mwisho kufika Gulu ilikuwa ni miaka ya zamani, utaanza tena kwa sababu serikali yake inatambua kwamba usafiri kwa gharama nafuu ni muhimu kwa ukuaji wa biashara.

Reli kutoka Malaba hadi Kampala, yenye urefu wa kilomita 273 ni muhimu pia kwa bidhaa za Uganda zinazouzwa nje ya nchi kupitia Bandari ya Mombasa.

Reli hiyo inapita katika wilaya tisa za Tororo, Butaleja, Iganda, Mayuge, Jinja, Buikwe, Mukono, Wakiso na Kampala.

Serikali imesema kwamba baada ya ukarabati wake, mizigo yote kutoka Bandari ya Mombasa, ambayo imekuwa ikisafirishwa kwa kutumia barabara, itasafirishwa kwa reli ili kupunguza gharama ya usafiri na ukarabati wa barabara kila mara.

Umoja wa Ulaya (EU) utasaidia serikali ya Uganda katika kufadhili ujenzi wa reli kutoka Tororo hadi Gulu, yenye urefu kwa kilomita 375.

Serikali ya Uganda pia imeanza mipango ya kufufua usafiri wa meli kutoka Kisumu Kenya hadi bandari za Kasensero na Bukakata.

*VOA*



Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alipokuwa kwenye kongamano kuhusu wanawake na siasa nchini Rwanda, lililofanyika Mei 17, 2010. **PICHA: AP**

# Rais Kenyatta azindua mchakato mabadiliko ya katiba

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amezindua rasmi mpango maalum wa kukusanya saini zitakazoanzisha mchakato wa kura ya maoni ili kufanyia marekebisho ya katiba.

Kinyume na ahadi ya Rais Kenyatta kuwa mchakato huo ni wa kuunganisha Wakenya wote, Makamu wa Rais, William Ruto na baadhi ya wabunge wanaomuunga mkono walisusia zoezi hilo.

Juhudi za Ruto za kupinga mageuzi ya katiba, kama inavyopendekezwa na Rais Kenyatta na aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, zinaonekana kugonga mwamba baada ya Rais Kenyatta kuzindua rasmi mchakato wa kukusanya sahihi ili kuidhinisha kura ya maoni ya kubadili katiba.

Ruto ambaye alikuwa mkosoaji wa mchakato huo wa kufanya mageuzi ya kikatiba hakuhudhuria hafla hiyo, sawa na wabunge wanaomuunga mkono ambao wote wamedai kuwa zoezi la kubadili katiba sio suala la dharura.

Lakini akiongea wakati wa hafla hiyo, Rais Kenyatta alisema mpango huo wa kubadilisha katiba unadhamiria kumaliza mizozo ya kisiasa ambayo imeshuhudiwa nchini Kenya kila baada ya uchaguzi mkuu.

Kuhusu tangazo la Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Upelelezi wa Jinai, George Kinoti, kuwa ameanzisha uchunguzi wa ghasia baada ya uchaguzi wa 2007/2008.

Hata hivyo, Rais Kenyatta ameshutumu hatua hiyo akisema hatakubali vitendo ambavyo vitafungua kile alichokitaja vidonda vya zamani na kuwaonya wale ambao wanataka kutumia machufuko yaliyofanyika kipindi cha nyuma kuzua uhasama na hali ya wasiwasi.

Hata hivyo, Wakenya wengi wanasema kuwa licha ya Rais Kenyatta kushinikiza kuidhinishwa kwa katiba mpya, wao hawajapokea nakala ya rasimu hiyo ya katiba au hawafahamu yaliyomo kwenye mapendekezo mapya.

Shughuli ya kukusanya saini hizo itaendelea kwa muda wa wiki moja kabla ya kuwasilisha kwa Tume ya Uchaguzi.

*BBC*

# Rwanda yaongoza duniani kwa usawa wa jinsia

**KIGALI, Rwanda**

IMEELEZWA kwamba Rwanda ndiyo nchi pekee duniani inayoongoza kwa kujali usawa wa kijinsia.

Rwanda, ambayo ni nchi ndogo ya Afrika Mashariki, inajivunia kwa sifa kubwa ya kuwa na idadi kubwa ya wanawake katika nafasi za kisiasa na serikalini.

Karibu theluthi tatu ya wabunge na asilimia 52 ya mawaziri ni wanawake. Spika wa Bunge chini ni mwanamke.

Wizara za Habari na Mawasiliano, Biashara na Viwanda zinaongozwa na wanawake.

Katiba ya Rwanda iliyoandikwa mwaka 2003, baada ya vita vya kimbari vya mwaka 1994 inatoa fursa kwa wanawake wengi kushiriki katika siasa, ikitaka asilimia 30 ya viti vya kisiasa kutengewa wanawake.

Wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake mwaka 2020, Rais wa Rwanda Paul Kagame, aliandika ujumbe wa twiter kwamba: "Kila wakati wanawake wanafanikiwa, nchi nzima inafanikiwa maendeleo hayawezi kupatikana bila ya kuwapo usawa wa kijinsia." Ifuatayo ni orodha ya nchi saba zinazoongoza kwa usawa wa kijinsia serikalini.

**Ethiopia**

Ethiopia ni nchi ya pili yenye idadi kubwa ya watu Afrika. Imechukua hatua madhubuti kuimarisha usawa wa kijinsia katika uteuzi wa maofisa serikalini tangu Waziri Mkuu Abiy Ahmed, alipoingia madarakani mwaka 2018.

Aliyekuwa mwanadiplomasia, Sahle-Work Zewde, alichaguliwa kuwa rais Oktoba 2018 na kuwa mwanamke wa kwanza kushikilia nafasi hiyo nchini humo.

Meaza Ashenafi aliteuliwa kuwa Jaji Mkuu Novemba mwaka 2018. Asilimia 45 ya mawaziri katika serikali ya Abiy Ahmed ni wanawake.

Wizara za Uchukuzi, Maendeleo ya Mijini na Ujenzi zinaongozwa na wanawake.

**Canada**

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Canada, Baraza la Mawaziri lilipata idadi sawa ya wanawake na wanaume miaka mitano iliyopita, Waziri Mkuu, Justin Trudeu, alipoanzisha utawala wa usawa wa jinsia.

Baraza la Mawaziri lina wanawake 18 na wanaume 18.

Naibu wa Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Fedha, Chrystia Freeland, ni mwanamke.

**Colombia**

Rais wa Colombia, Ivan Duque, alipoingia madarakani mwaka 2018, aliteua idadi sawa ya wanawake na wanaume katika Baraza la Mawaziri.

Hatua hiyo ilikuwa ya kwanza kuwahi kutokea nchini humo, ambapo kwa mara ya kwanza, mwanamke aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Kwa sasa, wanawake sita wanaongoza wizara mbalimbali kati ya baraza lake la mawaziri 16.

Marta Lucia Ramirez ni mwanamke wa kwanza kuwa Makamu wa Rais Colombia.

**Afrika Kusini**

Mnamo Juni, 2019, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisifiwa alipoteua baraza lake la mawaziri ambalo asilimia 47 ni wanawake, ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya nchi hiyo. Wizara 14 kati ya 28 zinaongozwa na wanawake.

**Iceland**

Iceland ina historia ya kuchagua wanawake kuwa kiongozi wa serikali, tangu mwaka 1980 wakati Vigdís Finnbogadóttir alipokuwa rais. Alikuwa madarakani hadi mwaka 1996. Iceland imeongozwa na wanawake kwa miaka 22 katika miaka 50 iliyopita.

**New Zealand**

Waziri Mkuu wa sasa, Jacinda Arden, alishinda uchaguzi mkuu Oktoba kwa kishindo. Bunge la New Zealand lina idadi kubwa ya wanawake. Baraza la Mawaziri lenye mawaziri 20, lina wanawake 8.

*VOA*

# KOEMAN

## AJITETEA GRIEZMANN KUANZIA BENCHI WAKISHINDA 4



**KIEV, Ukraine**

RONALD Koeman amedai hakuwa na sababu yoyote kwa uamuzi wake wa kutomwanzisha Antoine Griezmann, wakati Barcelona wakaiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Dynamo Kiev kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Mchezaji huyo wa Ufaransa aliwekwa benchi na aliingia kuchukua nafasi ya Philippe Coutinho dakika ya 66, na akafunga bao dakika za majeruhi.

Mahusiano ya Griezmann na nyota wa Barcelona, Lionel Messi, ambaye alipumzika kwa safari ya Ukraine, yamepamba vyombo vya habari kwa siku za hivi karibuni, baada ya kauli na wakala wake wa zamani ambaye ni mjomba wake.

Hata hivyo, Koeman alisema Griezmann alikuwa ana "furaha" pale Camp Nou na hana tatizo na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.

"Griezmann aliachwa benchi kwa sababu alikuwa na tatizo dogo na nilitaka kuwa na uhakika naye," alisema Koeman akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Ni muhimu sana kumpumzisha mchezaji ambaye anafanya kazi kwa bidii kubwa na anajifua sana kwenye mazoezi.

"Nimemwona (Griezmann) akijifua kwa nguvu tangu mwanzo. Ni mchezaji mwenye furaha, ambaye mara zote anataka kujitoa kwa ubora wake ili kuisaidia klabu."

Ushindi wa kikosi hicho cha Koeman dhidi ya Dynamo, kimeifanya Barcelona kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ALBA ATOA YA MOYONI KWA DOGO WA BARCA

**KIEV, Ukraine**



JORDI Alba amesema Sergino Dest anaweza kuwa nyota mkubwa sana wa Barcelona baada ya mlinzi huyo chipukizi kufunga bao lake la kwanza kwa klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani, alifunga bao la kwanza kwa 'Blaugrana' hao dhidi ya Dynamo Kiev, Jumanne wakati kikosi hicho cha kocha, Ronald Koeman kikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 na kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kutoka Kundi G.

Dest alionyesha kiwango cha juu kwenye safu ya ulinzi na alitengeneza pasi nzuri sita kwa kikosi hicho.

Mlinzi huyo wa kulia mwenye umri wa miaka 20, alimfanya Alba kufurahia zaidi kiwango chake na kuamua kutoa ya moyoni.

"Dest amekuja vizuri. Kwa sababu ya Sergi Roberto akiwa majeruhi nina uhakika atapata nafasi nyingi zaidi za kucheza," alisema Alba ambaye ni mlinzi wa kushoto wa Barcelona mara baada ya mchezo huo.

"Nafikiri yupo kwenye levo za juu kabisa na nina uhakika kama ataendelea kuwa kwenye kiwango hiki, sina shaka kwamba atakuwa nyota mkubwa sana hapa Barcelona."

Dest, aliyejiunga na Barca akitokea Ajax Oktoba, ameonyesha kubeba vizuri majukumu ya Sergi ambaye kwa sasa ni majeruhi.

Katika mchezo huo, Martin Braithwaite alifunga mara mbili na Antoine Griezmann moja na kuiwezesha Barca kupata ushindi wao wa nne kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## PSG IMESTAHILI USHINDI - TUCHEL



**PARIS, Ufaransa**

THOMAS Tuchel alisifia morali ya Paris Saint-Germain baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya RB Leipzig kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na alikataa kuomba radhi kwa kushinda vibaya.

PSG ambayo msimu uliopita ilicheza fainali ya michuano hiyo, hawakuwa kwenye kiwango cha kuvutia dhidi ya miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Jumanne, huku penalti ya Neymar ya dakika ya 11 ikiwapa ushindi huo.

Timu hiyo ilikuwa kwenye kiwango kibovu, kwani ilipiga mashuti matatu tu ya kulenga goli katika mchezo huo.

Matokeo hayo maana yake ni kwamba PSG sasa imeipiku Leipzig kwenye nafasi ya pili katika Kundi H wakiwa na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa huku zikiwa zimebaki mechi mbili.

Kocha aliye kwenye presha kubwa, Tuchel alisema timu yake ilistahili ushindi pale kwenye Dimba la Parc des Princes, lakini alikataa kusema samahani kwa kiwango kibovu cha timu.

"Tulikuwa na bahati na tulistahili ushindi, hilo ndilo pekee naweza kulisema kwa sasa," alisema kocha huyo akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Tulicheza kwa nguvu na wachezaji walikuwa na morali kubwa, na hata safu yetu ya ulinzi ndiyo ilikuwa moyo wa timu.

"La muhimu ni ushindi, siwezi kusema samahani kwa ushindi mbaya, hapana, tulistahili kushinda na tumeshinda."

## HABARI MICHEZO

# MORATA AANZA KUJIFUTUA JUVE

**TURIN, Italia**

ALVARO Morata anaamini yeye ni "zaidi ya mchezaji aliyekamilika" tangu aliporudi Juventus, baada ya kuifikia rekodi yake ya mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Morata alifunga bao lake la tano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kichwa wakati Juventus wakiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Ferencvaros, na kupata nafasi ya kutinga hatua ya 16-bora kwenye michuano hiyo kutoka Kundi G.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, amekuwa kwenye kiwango bora zaidi tangu aliporudi tena Juve, ambako alitumia misimu miwili kati ya mwaka 2014 na 2016 na alifunga mabao 15 kwenye Serie A na kutoa pasi za mwisho 12 kwa kipindi hicho.

Msimu wa 2014-15, alifunga mabao matano sawa na sasa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya - wakati Juve ilipotinga fainali na ikafungwa na Barcelona.

Baada ya kuifikia rekodi yake hiyo katika mich- ezo minne tu, Morata ambaye shuti lake liligonga mwamba wakati akiingia akitokea benchi pale Turin, alidai amekuwa mshambuliaji bora zaidi kwa sasa.

"Hakuna kilichobadilika kwangu, nimesema mara nyingi, unajifunza kutoka kwenye kipindi chako cha uchezaji.

"Mimi ni zaidi ya mchezaji niliyekamilika sasa," alisema straika huyo wa zamani wa Atletico Madrid, Chelsea na Real Madrid akiiambia Sky Italia.

"Wakati nilipokuwa na umri wa miaka 22, nilikuwa nasubiri tu mpira uje upande wangu, lakini sasa ninauwezo wa kutafuta mpira kutoka sehemu yoyote.

"Nilikuwa na nafasi nyingine ya kufunga wakati nilipogonga mwamba. Nilikuwa na bahati kwa kufunga bao lile, lakini nikakosa nafasi nyingine."

Katika mchezo huo, Cristiano Ronaldo alifunga la kwanza dakika ya 35 akisawazisha lile la Myrto Uzuni aliowafungia Ferencvaros, na aliifikia rekodi ya Lionel Messi ya kufikisha mabao 70 aliyofunga dimba la nyumbani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.



# HAALAND
## AVUNJA REKODI UEFA

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland ameweka rekodi mpya ya kufikisha haraka zaidi mabao 15 kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kufunga bao la ufunguzi dhidi ya Club Brugge.

Nyota huyo wa Borussia Dortmund, tayari aliweka rekodi ya kufunga mabao 10 katika mechi tano, sasa ameipiku rekodi ya Ruud van Nistelrooy na Roberto Soldado.

Haaland aliiweka Dortmund mbele kwa bao 1-0 katika dakika ya 18 kwenye mchezo huo dhidi ya Brugge.

Bao hilo lilimfanya kufikisha mabao 15 kwenye mashindano hayo ya Ulaya kwa mechi 12 tu, akiwa pia amefurahia mwanzo mzuri kuanzia kule klabu ya Salzburg msimu uliopita.

Awali rekodi hiyo ya kufunga mabao 15 kwa haraka zaidi iliwekwa na nyota wa zamani wa Uholanzi na Manchester United, Van Nistelrooy na nyota wa zamani wa Valencia, Soldado ambao walifikisha idadi hiyo ya mabao katika mechi 19.



# FERNANDES AMBEBA RASHFORD MABINGWA ULAYA

**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes aliacha kupiga penalti wakati akiwa na uwezo wa kufunga 'hat-trick' dhidi ya Istanbul Basaksehir, ili kumsaidia Marcus Rashford kubaki kuwa mmoja wa wachezaji wanaoongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Manchester United iliifunga Basaksehir mabao 4-1 pale kwenye dimba la Old Trafford na hivyo kuendelea kuwa kinara wa Kundi H, huku zikiwa zimebaki mechi mbili dhidi ya Paris Saint-Germain na RB Leipzig.

United inahitaji pointi moja tu kutoka mechi hizo mbili ili iweze kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16-bora kwenye mashindano hayo.

Fernandes alifunga mara mbili ndani ya dakika 19 - na alikuwa na nafasi ya kufunga bao lake la tatu kwenye mchezo huo wakati Boli Bolingoli alipomfanyia faulo Rashford eneo la hatari.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mara zote ndiye mpigaji penalti wa United, awali alichukua mpira, lakini akampatia Rashford, ambaye alifunga.

Rashford ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa England hilo lilikuwa bao lake la tano kwenye mashindano hayo msimu huu.

Na Fernandes aliamua kumpatia penalti hiyo apige ili kuweza kupata mabao mengi kwenye michuano hiyo.

"Bila shaka, kila mchezaji anataka kufunga hat-trick, lakini baada ya mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya (West Brom Jumamosi) nilimwambia Rashford kwamba anapiga inayofuata," alisema Fernandes akiiambia BT Sport.

"Hivyo, nilikumbuka hili na pia yeye ni mmoja wa wafungaji wanaoongoza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo nilifikiria ni muhimu kwa yeye kuendelea kufunga ili aweze kujiamini zaidi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GIROUD SASA AMTESA LAMPARD CHELSEA

●●●Nina tatizo kwa sasa, kwa sababu Abraham anacheza vizuri na Olivier naye yuko kwenye...

**LONDON, England**

KOHA wa Chelsea, Frank Lampard amemsifia Olivier Giroud kwa mara nyingine kwa kufunga bao la ushindi dakika za majeruhi dhidi ya Rennes na kusema straika huyo amempa "tatizo " wakati linapokuja suala la kuchagua timu.

Giroud aliyeingia kipindi cha pili, alifunga bao la ushindi kwa Chelsea juzi, Jumanne wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 na kuiwezesha timu yake kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kutoka Kundi E.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alifunga bao hilo pale kwenye dimba la Roazhon Park, likiwa ni la pili kwake katika mechi nane za ugenini msimu huu.

Lampard alipaza sauti kumsifia Giroud, huku akisema kwa sasa mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal amemweka kwenye tatizo kubwa la kuchagua kikosi cha kwanza.

"Anafanya mambo kama alivyofanya usiku wa leo (juzi), ni mchezaji muhimu kwa upande wetu," alisema Lampard akiiambia BT Sport baada ya mchezo huo.

"Bao lake lilikuwa muhimu sana kwa timu, na hasa ukizingatia uchezaji wake na namna anavyojituma uwanjani.

"Nina tatizo kwa sasa, kwa sababu Tammy (Abraham) anacheza vizuri na Olivier naye yuko kwenye kiwango cha kuvutia.

"Nina wachezaji wawili ambao wanapigania nafasi moja uwanjani, lakini ni tatizo zuri kwa upande wangu.

"Atapata dakika kwa sababu ya idadi ya mechi. Uliona namna bao lake lilivyoleta hisia, kwa sababu lilikuwa la dakika za majeruhi."

Giroud amefunga mabao sita kwenye mechi 13 tangu Ligi Kuu iliporudi Juni- na moja zaidi ya Abraham, ambaye amecheza mechi nne zaidi.

## KWA UFUPI

**LAPORTA ATAKA URAIS BARCA**

RAIS wa zamani wa Barcelona, Joan Laporta anajiandaa kutangaza kugombea tena nafasi hiyo ya urais kwenye uchaguzi ujao wa miamba hiyo ya Hispania. ***(Marca)***

**ARSENAL, EVERTON VITANI**

ARSENAL inamfuatilia kinda wao wa zamani, Yunus Musah, 17, wakati huu Everton, Leeds na Wolves pia zikivutiwa na winga huyo wa Valencia, ambaye ni raia wa Marekani. ***(90 min)***

**CHELSEA YANOGEWA NA THIAGO**

CHELSEA tayari ipo katika mazungumzo na beki Mbrazil Thiago Silva, 36, kuhusu kuongeza mkataba wake kwa mwaka mmoja zaidi hadi 2022. ***(Tuttomercato - in Italian)***

**'VARANE AHAMISHIKI MADRID'**

REAL Madrid imejibu tetesi zinazomhusu Raphael Varane kuhusishwa na Manchester United kwa kueleza kuwa beki huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 27, "ahamishiki". ***(Sun)***

**PEPE KIKAANGONI ARSENAL**

ARSENAL inajiandaa kuzungumza na Nicolas Pepe baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu kwenye mechi dhidi ya Leeds Jumapili, lakini haipo tayari kumtoa kwa mkopo straika huyo wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la Januari. ***(Times)***

**BOATENG KUTOSWA BAYERN**

BAYERN Munich imeamua kutompa tena ofa ya mkataba mpya Jerome Boateng, 32, wakati huu wa sasa wa beki huyo wa Ujerumani utakapomalizika majira ya joto yajayo. ***(Sport Bild - in German)***

**ERIKSEN APOTEZEWA ARSENAL**

ARSENAL haina mpango wowote wa kwenda kumsajili kiungo wa Inter Milan, Christian Eriksen, 28. Borussia Dortmund na Paris St-Germain pia zimekuwa zikihusishwa na nyota huyo wa kimataifa wa Denmark. ***(Star)***

**SCHOLES APONDA USAJILI UTD**

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Paul Scholes, amesema "kumekuwa na wachezaji wengi" ambao kocha wa zamani wa miamba hiyo ya Old Trafford, Sir Alex Ferguson asingeweza kuwasajili, kauli hiyo akiitoa wakati akihoji sera za usajili za klabu hiyo kwa sasa. ***(BT Sport, via Star)***

**MARTINEZ KUFUNGWA INTER**

INTER Milan inataka kujihakikishia inakamilisha kumwongeza mkataba Lautaro Martinez, 23, kabla ya dirisha la usajili la Januari baada ya straika huyo wa kimataifa wa Argentina kuivutia Barcelona majira ya joto yaliyomalizika. ***(Sport)***

**MODRIC ATAKA KUSTAAFIA REAL**

KIUNGO Mcroatia, Luka Modric, 35, yupo tayari kubaki Real Madrid na kustaafia kwa miamba hiyo ya Hispania, wakati huu mkataba wake ukitarajiwa kumalizika majira ya joto yajayo. ***(Marca)***

**MAICON KUTUA SERIE D**

NYOTA wa zamani wa Inter Milan, Manchester City na beki wa kulia wa Brazil, Maicon, 29, yupo kwenye mazungumzo kuhusu kujiunga na timu ya Italia inayoshiriki Serie D, Sona. ***(Padova Sport - in Italian)***

**ARSENAL KUMRUDIA BERGE**

ARSENAL inavutiwa na kiungo wa Sheffield United, Sander Berge, licha ya kuikosa saini ya Mnorway huyo mwenye umri wa miaka 22, wakati ilipotaka kumsajili nyota huyo wa Bramall Lane katika dirisha la Januari lililopita. ***(VG - in Norwegian)***

HABARI MICHEZO

# MOROCCO ATOA HESABU ZA KUWAMALIZA WASUDAN CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemedi Morocco, amepania kuiongoza timu hiyo kumalizia mchezo wao nyumbani wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Al Rabita FC ya Sudan Kusini, ameeleza.

Namungo itaanzia nyumbani kwa kukuwakaribisha Wasudan Kusini hao Jumamosi katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam kabla ya timu hizo kurudiana Desemba 4, mwaka huu nchini Sudan Kusini.

Mshindi wa jumla katika mechi hizo mbili atasonga mbele kwenye michuano hiyo ya pili kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo kwa Tanzania msimu huu inawakilishwa na Simba.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanya Uwanja wa Uhuru, Morocco alisema anahitaji kumaliza mechi hiyo mapema wakiwa nyumbani Jumamosi.

Alisema atakatumia mbinu kali zaidi ya alizotumia katika mechi iliyopita ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga, ili kupata matokeo mazuri na kuhakikisha anamaliza mchezo akiwa nyumbani kabla ya kwenda kurudiana ugenini.

"Natakiwa kumaliza mechi mapema, kizuri zaidi tunaanzia nyumbani, saikolojia ya wachezaji wangu ipo vizuri, kikubwa ni kuendelea kufanyia kazi upungufu mdogo mdogo katika safu ya ushambuliaji," alisema Morocco.

Naye kipa wa Namungo na timu ya Taifa ya Burundi, Jonathan Nahimana, alisema wamejiandaa vizuri na wako fiti kukabiliana na wapinzani wao hao.

"Kila mmoja wetu yupo vizuri na tuko fiti kwa ajili ya mechi hiyo, tutahakikisha tunapambana kumaliza mapema mechi yetu ya kwanza tukiwa nyumbani," alisema Nahimana.

Alisema kwa uzoefu wake wa michuano ya kimataifa, ana imani atasaidiana na wenzake kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ya mechi ya nyumbani.

## Hitimana anukia viatu vya Katwila Mtibwa

**Na Saada Akida**

HUKU juzi ikikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Polisi Tanzania, uongozi wa Mtibwa Sugar, umesema upo katika hatua za mwisho kukamilisha mchakato wa kumpata kocha mkuu wa kigeni atakayechukua nafasi ya Zuber Katwila aliyetimkia Ihefu FC ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, aliyekuwa Kocha Mkuu wa Namungo FC ya Ruangwa mkoani Lindi, Mnyarwanda Thierry Hitimana, amekuwa akitajwa kuwa anaongoza mbio hizo za kuteuliwa kuwanoa 'Wakata Miwa' hao wa Manungu.

Nipashe lilipomtafuta Hitimana kujua endapo ni miongoni mwa walioomba nafasi hiyo, ama kuwa na mazungumzo na miamba hiyo ya Manungu, hakupatikana jana, hata hivyo juhudi za kumtafuta bado zinaendelea.


Lakini akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkurugezi Mtendaji wa Mtibwa Sugar, Jamal Bayser, alisema walikuwa katika mchakato wa mchujo wa kupitia wasifu (CV) za makocha mbalimbali ndani na nje ya Tanzania walioomba nafasi hiyo na sasa unakaribia kufikia mwisho.

Alisema katika mchujo huo wamebaki na CV sita za makocha wakigeni, ambao wanawajadili ili kupata jina la kocha mmoja atakayechukuwa nafasi hiyo ya Katwila.

"Tunaendelea na mchakato wetu wa kupitia CV sita za makocha wa kigeni ambao tumekuwa tukiwajadili, hadi mzunguko wa pili tuwe tumepata kocha mkuu," alisema Bayser.

Alisema hawezi kuweka wazi majina ya makocha hao kwa sababu bado wanaendelea na mchakato huo wa kutafuta mrithi wa Katwila.

HUUPATI...



Mshambuliaji wa Manchester United, Edinson Cavani (Kulia), akipata upinzani dhidi ya beki wa zamani wa Liverpool, kwa sasa Istanbul Basaksehir, Martin Skrtel, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford, juzi usiku na United kushinda 4-1. **HABARI UK. 21**

## JKT Tanzania na gundu la nyumbani

**Na Adam Fungamwango**

KIPIGO cha bao 1-0 ilichokipata JKT Tanzania juzi Jumanne dhidi ya timu dhaifu ya Mbeya City, kimeendeleza rekodi yao mbovu ya kutopata ushindi wowote kwenye uwanja wake wa nyumbani tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

JKT Tanzania ilicheza mechi hiyo kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa, ambao kwa sasa inautumia kwa muda kama wa nyumbani, mpaka hapo itakapotaarifiwa rasmi na Bodi ya Ligi kurejea kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma ambao nao pia haijawahi kushinda licha ya kucheza mechi kadhaa.

Kati ya mechi 12 ambazo JKT Tanzania imecheza, sita imecheza kwenye uwanja wa nyumbani na haijashinda hata moja, ikitoka sare mechi moja tu na kupoteza tano.

Ikiwa nyumbani, ilichapwa mabao 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji, ikabamizwa 4-0 na Simba, kisha bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya Gwambina FC, kabla juzi kukubali kulala kwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City. Mechi pekee ambayo ilipata sare nyumbani, ilikuwa ni ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

## Zuchu sasa balozi bidhaa za Tridea

**Na Faustine Feliciane**

NYOTA ya msanii wa Bongo Fleva, Zuhura Othman 'Zuchu', imezidi kung'ara baada ya jana kutangazwa kuwa balozi mpya wa Kampuni ya Urembo ya Tridea ya jijini Dar es Salaam.

Zuchu ambaye ni msanii wa muziki wa Bongo Fleva katika Lebo ya WCB, atakuwa balozi wa bidhaa za Tridea akihusika kwenye matangazo ya TV, magazeti na mitandao ya kijamii.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Grace Luswaga, alisema wameamua kufanya kazi na Zuchu baada ya kuona kazi zake zinakubalika na atakuwa balozi mzuri kwa wengine.

"Zuchu ni msanii wa kike anayekubalika kwa sasa na atakuwa balozi mzuri kwa wengine kupitia bidhaa zetu ikiwamo kuwasaidia wanawake kutumia na kujisikia vizuri," alisema.

Kwa upande wake Zuchu alisema: "Nina furaha kuingia mkataba na Tridea Cosmetics, nitakua balozi mzuri kwa wanawake wenzangu na kina dada, mama yangu pia anatumia bidhaa hizi na mimi tangu nikiwa mdogo nimekuwa nikizitumia," alisema Zuchu.

# Michezo

Alhamisi Novemba 26, 2020

Nipashe




GIROUD SASA AMTESA LAMPARD CHELSEA

HABARI UK 22

TUMEWAFIKIA...



Wachezaji wa Simba wakiingia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Boli Addis Ababa, Ethiopia, jana asubuhi tayari kuunganisha ndege ya kwenda Abuja, Nigeria kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji, Plateau United utakaopigwa Jumapili katika Uwanja wa New Jos nchini humo. Kikosi hicho kiliwasili salama Nigeria jana mchana. **PICHA: SIMBA**

## MOROCCO: HESABU WASUDAN CAF HIZI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemedi Morocco, amepania kuiongoza timu hiyo kumalizia mchezo wao nyumbani wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Al Rabita FC ya Sudan Kusini, ameeleza.

**UK. 23**

## HAALAND AVUNJA REKODI MABAO UEFA



**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland ameweka rekodi mpya ya kufikisha haraka zaidi mabao 15 kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kufunga bao la ufunguzi dhidi ya Club Brugge.

**UK. 21**

# SIMBA 'FULU MZUKA' NIGERIA

●●●Yajichimbia Abuja ikipanga kuwashtukiza Plateau Jumamosi kabla ya kushuka dimba Jumapili, uongozi wasema...

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Simba, tayari wametua mjini Abuja, Nigeria wakiwa na ari kubwa ya ushindi kuelekea mchezo wao wa kwanza wa hatua ya awali dhidi ya Plateau United kuwania kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani humu katika ngazi ya klabu.

Simba ambayo iliondokea Uwanja wa Ndege wa KIA Jumanne kwa 'mwewe' wa Shirika la Ndege la Ethiopia, ililala Addis Ababa, Ethiopia kabla ya kuondoka jana asubuhi na mchana kutua salama Abuja, Nigeria ikiwa na kikosi chake cha wachezaji 24 tayari kwa mechi hiyo itakayopigwa Jumapili katika Uwanja New Jos uliopo mji wa Jos nchini humo.

Akizungumza na Nipashe baada ya timu hiyo kuwasili Nigeria jana mchana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba (CEO), Barbara Gonzalez, alisema wataweka kambi Abuja na timu itaondoka mjini hapo Jumamosi kuelekea Jos ambapo ni umbali wa kilometa 181 kutoka Abuja mwendo wa saa tatu kama ukitumia basi.

"Tunashukuru tumefika salama na wachezaji wote wapo fiti, tunatarajia kuweka kambi mjini hapa (Abuja) hadi Jumamosi ambapo tutasafiri kuelekea Jos mji ambapo mechi yetu itachezwa," alisema Barbara.

Kuhusu mechi hiyo kuchezwa Jumapili na si Ijumaa kama ambavyo ilikuwa ikifahamika na mashabiki wengi wa Simba hapa nchini, Barbara alisema ratiba hiyo haijabadilishwa na kwamba wao walikuwa wanafahamu kuwa mechi hiyo inachezwa Jumapili.

"Hapana si kweli, hakuna mabadiliko yoyote, mechi ni Jumapili kama ambavyo ilikuwa imepangwa," alisema huku akieleza kuwa hali ya hewa ya Abuja haina tofauti sana na ya Dar es Salaam.

"Hapa Abuja hali ya hewa haitofautiani sana na Dar es Salaam kwa sasa, ila kwa Jos nasikia huko kuna baridi kidogo, hivyo tutaelekea huko Jumamosi ama vinginevyo Ijumaa."

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, tayari alishaeleza malengo yao ya kufika hatua ya makundi kwanza kabla ya kufikiria nusu fainali ya michuano hiyo msimu huu.

Licha ya Sven kueleza tayari ameshadokezwa na watu wake wa karibu namna wapinzani wao hao wanavyocheza, amewataka wachezaji wake kujituma na kuhakikisha wanapata ushindi ugenini ili kupunguza presha kwenye mechi ya marudiano Desemba 4, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

"Kikubwa ni kupata ushindi ugenini kwanza ili kuondoa presha kwenye mechi ya marudiano, tunajua haitakuwa rahisi kwa kuwa Plateau nao watataka kupata matokeo nyumbani, lakini ninaamini hilo linawezekana kama wachezaji wakitumia vema kila nafasi," alisema.

Endapo Simba itaitoa Plateau itakutana na mshindi wa jumla kati ya CD Costa do Sol ya Msumbiji ama FC Platinum ya Zimbabwe katika raundi inayofuta na ikivuka hapo itatinga moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002